# Kulawa
# Ulongozi

Chitabu cha Kulawa chosimulila simulizi isongele muna ichitabu cha Mwanduso yoilonga mbuli ya lukolo lwa Bulahimu. Chitabu chino chotangigwa Kulawa kwa viya cholaagusa kusonhela viya Waisilaili viwalawile Misili na kubwela isi ija Mulungu iyamulaganile Bulahimu. Kwa kusondelela mahokelo, wasomi wohuwila kuwa hanhu hakulu ha chitabu chino handikigwa na mulotezi Musa, mbuli ino yolongigwa mbaka na chitabu chanyewo. Kulawa 24:4 yolonga viya Musa viyandike hanhu hamwenga muna ichitabu chino. Chifungu muna ichitabu cha Yoshua 8:31 chotambula lagilizo dili muna ichitabu cha Kulawa 20:25 na kulonga, “fana viyandikigwe muna ichitabu cha malagilizo ya Musa.” Vitabu va Lagano da Sambi votambula vitabu vandikikwe na Musa, mfano Lagano da Sambi vodilonga mbuli ya chibago chikwaka moto bila kulungula, dolonga kuwa mbuli ino yandikigwa muna, “ichitabu cha Musa” (Maliko 12:26). Yodahika Waisilaili walawa muna iisi ya Misili hagati ya mwaka 1,300 hebu 1,400 KK (Inghali Chilisito). Muna ichitabu cha 1 Wafalume 6:1 ilongigwa Waisilaili walawa Misili miyaka 480 ing'hali hainafika mwaka wa nne wa kutawala kwake Mfalume Suleimani.

Chitabu cha Kulawa chokanhamiza viya viyatendile Mulungu muladi kugendesa waminika wake kusonhela chilagano chiyawalaganile Bu-

lahimu na Isaka na Yakobo. Chitabu chosimulila sang'hano ng'hulu za ukombola wa Mulungu kwa welesi wa Bulahimu niiwawo Waisilaili, viwakalile wolawa muna iisi ya Misili (Kulawa sula ya 1 mbaka 12). Kulawa uko Mulungu kawalongoza wanhu wake mbaka kuna yamabawe yakalile hasi ya mulima Sinai hanhu haja Mulungu hoyamwing'hile Musa Malagilizo mengi muladi Waisilaili wayasondelele (Kulawa sula ya 12 mbaka 19). Malagilizo yano yolonga viya viwalondeke kusang'hana, viya viwalondeke kulava nhambiko, na mbuli zozilonga kusonhela uzenzi wa hema da mting'hano (baho hanhu hayakalile Mulungu hagati yawo) hamwe na sanduku da Lagano na via vimwenga va nhambiko muna dihema da mting'hano, na mawalo malumu ya wakulu wa nhambiko (Kulawa sula ya 20 mbaka 31). Maabaho viumalile wihi wihile haja Waisilaili viwaitendele nyang'hiti ya ng'ombe wa zahabu, Musa kaiting'hana na Mulungu kaidi (Kulawa sula ya 32 mbaka 33). Kuuhelelo wa chitabu chino chosoma via vitambuligwe ichanduso vovitendigwe (Kulawa sula ya 33 mbaka 40).

**Mbuli zilimuno**

1. Muna isula ya 1 yolonga viya wana wa Isilaili viwagumigwe muna uutumwa muna iisi ya Misili.
2. Muna isula ya 2 mbaka 4 zomtambula Musa na kusimulila ugima wake kwandusila udodo wake mbaka viyatangigwe kuwakombola wanhu wa Mulungu.
3. Maabaho mwandikaji kosimulila viya Mulungu viyatendile mauzauza na kuitowa isi

ya Misili kwa mahulo makulu kwa lungilo da kuwakombola wanhu wake kulawa muna iisi ija na kulawa kwa wakalizi wa mfalume wa Misili. (Sula ya 5 mbaka 15:21).

4. Kulawa hano wanhu wa Isilaili wandusa mwanza na wafika kuna umulima Sinai (sula ya 15:22 mbaka sula 19).
5. Muna isula ya 20 mbaka 31 chosoma viya Mulungu viyamwing'hile Musa Malagilizo, malagilizo yalongile wanhu wa Mulungu, Waisilaili viwolondeka kukala na kutambika.
6. Muna isula ya 32 yandikigwa viya wana wa Isilaili viwamulekile Mungu kwa kumsongeza ndugu wa Musa yoyatangigwe Haluni yawatendele nyang'hiti ilingile fana ng'ombe wa zahabu.
7. Sula ya 33 mbaka 40 zolonga viya Musa viyauwonile utunhizo wa Mungu na kuwafunza Waisilaili malagilizo ya Mungu, hamwe na kuwalongela voilondeka kuzenga hema da mting'hano na sanduku da lagano na via vimwenga va nham biko hana dihema da mting'hanila na mbuli za mawalo ya wakulu wa nhambiko.

### *Waisilaeli wogazigwa muna iisi ya Misili*

1 Yano ni mazina ya wana wa Yakobo yoy-
atangigwe Isilaili wowahitile Misili hamwe nayo,
2 Lubeni na Simeoni na Lawi na Yuda, 3 Isakali
na Zabuloni na Benjamini na 4 Dani na Nafutali
na Gadi na Asheli. 5 Welesi wose wa Yakobo
ukala malongo saba, lusita ulwo Yosefu kakala
yokala uko Misili. 6 Maabaho hamwande Yosefu
kadanganika, iviya na ndugu zake na welesi wose

wadanganika, 7 Mbali welesi wa Isilaili wakala
wokweleka na kongezeka ng'hani, wakala wengi
ng'hani na wagendelela kongezeka ludabwa, ivo
isi ija ya Misili ikala wenela wawo. 8 Maabaho
kalawilila mfalume wa imwenga, kuitawala Mis-
ili yohammanyile Yosefu.

9 Kawalongela wanhu wake, “Loleni wanhu wa
Isilaili ni wengi ng'hani na wana ludabwa kufosa
cheye. 10 Cholondeka chizahile nzila ya ubala
sekewongezeke, one siivo, ihalawilila ng'hondo
wezailumba na wehi wetu na kuitowa na cheye
na kusegela mwiisi.” 11 Ivo Wamisili waweka
wemilizi wawemilize Waisilaili na kuwagaza kwa
sang'hano ndala ya kumzengela mfalume wa Mis-
ili mabululu ya ngama uko Pisomo na Lamasesi.
12 Mbali kwaviya Wamisili viwawagazile Waisi-
laili, niivo viwongezeke na kwenela. Wamisili
wawadumba Waisilaili, 13 na wawatendela usede
wanhu wa Isilaili. 14 Wautenda ugima wawo
wihe kwa sang'hano ndala, sang'hano ya kutenda
chokaa na kutengeneza matafali na sang'hano
zose za muna imigunda. Sang'hano izo zose,
Waisilaili wasang'haniligwa kwa usede.

15 Maabaho mfalume wa Misili kawalongela
walala wowataza wanaake wa Chiebulaniya
kweleka, imwe zina jake katangigwa Shifila
na wekaidi zina jake katangigwa Pua.
16 Kawalongela, “Muhawataza wanaake
wa Chiebulaniya kuna ukuibasula, one
yahavumbuka mwana wa chilume mkomeni,
mbali one yahavumbuka mwana wa chike
mulekeni.” 17 Mbali walala wamdumba Mulungu

na hawatendile fana viyawalagilize mfalume
wa Misili, wawaleka wana wa chilume wakale.
18 Maabaho mfalume wa Misili kawatanga walala
waja na kawauza, “Habali mutenda vino? Habali
muwaleka wana wa chilume wakale?” 19 Walala
wawo wamwidika mfalume wa Misili, “Wanaake
wa Chiebulaniya hawalingile fana wanaake
wa Chimisili bule, woibasula himahima, na
wana wawo wokwelekigwa yang'hali mulala
hanafika.” 20 Ivo Mulungu kawatendela yanogile
walala wawo, na wanhu wongezeka ng'hani,
wagendelela kuwa na ludabwa ng'hani. 21 Na
kwaviya walala wawo wamdumba Mulungu,
Mulungu kaweng'ha welesi wawo wenyewo.
22 Maabaho mfalume wa Misili kawalagiliza
wanhu wake wose, “Chila mwana wa chilume
yondayelekwe kwa Waebulaniya yasigwe muna
ulwanda lwa Naili, mbali chila mwana wa chike
mulekeni.”

# 2

## *Kwelekigwa kwa Musa*

1 Siku izo munhu kulawa kabila da Lawi kasola
muke wa kabila jake mwenyewo, 2 nayo kapata
wimo na kaibasula mwana wa chilume. Viyamu-
wone kuwa kakala mwana yanogile ng'hani, kam-
fisa kwa miyezi mitatu. 3 Mbali viyapotwile kum-
fisa kampatila chigelo cha mayani na kachibu-
lugiza tulasi, kamwika mgati yake na kuchika
hana yamayani yokota muna ulwanda lwa Naili.
4 Lumbu jake imwana kema hatali hainzila mu-
ladi yadahe kulola chiya chondachimulawilile.

5 Mwana wa chike wa mfalume wa Misili
kahumuluka kuulwanda yoge, na wasang'hani
wake wakala wogenda genda mumgwazo ya
ulwanda. Viyawone ichigelo muna yamakengega,
kamtuma msang'hani wa chike yachisole.
6 Kachivugula na kawona mwana wa chilume.
Kakala kolila, ivo kamuwonela ubazi na kalonga,
"Ino ni imwe wa wana wa Chiebulaniya."

7 Maabaho lumbu wa imwana kamuuza mndele
wa mfalume wa Misili, "Nihite nikamtange muke
wa kumong'heza imwana mwa wanaake wa
Chiebulaniya?" 8 Mndele wa mfalume wa Misili
kamwidika. "Wona." Ivo imndele kahita na kam-
gala mami yake imwana. 9 Mndele wa mfalume
wa Misili kamulongela mwanamke ija, "Msole
imwana ino unyong'hezele, nizakuliha." Ivo
mwanamke ija kamsola imwana kamong'heza.
10 Hamwande mwana viyakulile kamgala kwa
mndele wa mfalume wa Misili, nayo kamtenda
kuwa mwanage. Mndele wa mfalume kalonga,
"Nimulava muna yamazi." Ivo kamtanga zina
jake Musa.

### *Musa kokimbilila Midiyani*

11 Siku izo Musa viyakulile kahita kuwalaula
ndugu zake Waebulaniya na kulola sang'hano
zawo ndala ziwotenda. Kawona Mmisili kom-
towa Muebulaniya, imwe wa ndugu zake. 12 Musa
kalola banzi zose, na viyawone kuwa habule
munhu yomuwona, kamkoma Mmisili ija na
lukuli lwake kalufisa muna umsanga. 13 Igolo
yake kahita kaidi na kawona Waebulaniya waidi
woitowa. Kamulongela ija yabanange, "Habali
komtowa Muebulaniya miyago?"

14 Munhu ija kamwidika, “Yelihi yakutendile
weye kuwa mtawala wetu na msemi? Vino
kolonda unikome fana viya viumkomile Mmisili
ija?” Maabaho Musa kadumba na kaiuzag-
iza mwenyewo, “Vino wanhu wavimanya chiya
chinitendile?” 15 Mfalume viyahulike yaja yalaw-
ilile, kalonda kumkoma Musa, mbali Musa kam-
banga mfalume wa Misili na kahita kukala muna
isi ya Midiani.

Siku dimwe Musa kakala hamgwazo wa
disima. 16 Mkulu wa nhambiko wa Midiani
kakala na wandele saba, nawo weza kudeha
mazi. Wamemeza mbaluti muladi wadahe
kuwang'wiza ng'hondolo na luti wa tati yawo.
17 Wadimi weza na wawawinga wandele waja
saba, mbali Musa kema na kuwataza kuding'wiza
bumbila da wanyama wawo. 18 Viwabwelile
kwa tati yawo Leueli, kawauza, “Habali diyelo
hamkalame bule kubwela?”

19 Wamwidika, “Mmisili kachilopola na
wadimi, na iviya kachidehela mazi na kung'wiza
wanyama wetu.”

20 Kawauza wandele wake, “Munhu iyo
kakulihi?” “Habali mumuleka uko munhu iyo?
Hiteni mukamgoneke yaje na cheye.”

21 Musa katogola kukala haja, Yesilo
kamwing'ha Musa mndele wake yatangigwe
Sipola yamsole. 22 Sipola kamwelekela
mwana wa chilume. Musa kailongela
mwenyewo, “Nitogoligwa kukala muna iisi iyo ya
manyambenyambe.” Ivo kamtanga mwana iyo
zina Gelishomu.

23 Viifosile miyaka mingi mfalume wa Misili
kadanganika, mbali Waisilaili wakala wang'hali
muna utumwa na wolilila kutazigwa. Kugutilila
kwawo kumfikila Mulungu. 24 Mulungu kahulika
ndilo yawo na kakumbuka lagano diyekile na Bu-
lahimu na Isaka na Yakobo. 25 Mulungu kawalola
Waisilaili na kavimanya viya viwogaya.

# 3

*Mulungu komtanga Musa*

1 Siku dimwe Musa viyakalile yodima
ng'hondolo na luti wa Yesilo mkoi wake, mkulu
wa nhambiko wa Midiani, kadilanguliza bumbila
kufosa uswelo wa zuwa muna ichuwala kuhita
Holebu, kuna mulima wa Mulungu. 2 Msenga
wa Mndewa Mulungu kamulawilila Musa muna
dilambi da moto muna ichibago. Musa kawona
ichibago chokwaka moto mbali hachitakamile.
3 Musa kalonga, "Yano mauzauza, habali
chibago chokwaka moto na hachitakamila?
Nizachikwenhukila nikachilole."

4 Mndewa Mulungu viyawone kuwa Musa kok-
wenhuka habehi, kamtanga kulawa hagati ya
ichibago na kalonga, "Musa! Musa!"

Musa kamwidika "Wona, nabaha."

5 Mndewa Mulungu kamulongela, "Sekeukwen-
huke habehi. Vula vilatu vako, kwaviya howimile
ni hanhu helile." 6 Maabaho kalonga, "Niye ni Mu-
lungu wa wasaho zako, Mulungu wa Bulahimu na
Isaka na Yakobo." Ivo Musa kaigubika chihanga
chake, kwaviya kadumba kumulola Mulungu.

7 Maabaho Mndewa Mulungu kalonga, "Kweli
niyawona manhesa ya wanhu wangu weli muna

iisi ya Misili. Nihulika ndilo yawo kwa ichimu cha wemilizi wa Misili. Niumanya usungu wawo.
8 Ivo nihumuluka muladi niwakombole muna imikono ya Wamisili, nizawalava umo na kuwagala kuna isi ino inogile na ng'hulu, isi ili na ulongo unogile, isi ya Wakanaani na Wahiti na Waamoli na Wapelizi na Wahivi na Wayebusi.
9 Lelo kulila kwa wanhu wangu Waisilaili kunifikila niye. Niwona viya Wamisili viwowagaza.
10 Lelo hita nokutuma kwa mfalume wa Misili muladi ukawalave wanhu wangu wana Isilaili muna iisi ya Misili."

11 Mbali Musa kamulongela Mulungu, "Niye yelihi mbaka nidahe kuhita kwa mfalume wa Misili na kuwalava Waisilaili muna iisi ya Misili?"

12 Mulungu kamulongela, "Nizakuwa hamwe na weye. Na chino chizakuwa chilaguso kuwa niye iyo nikutumile. Vondauwalave wanhu muna iisi ya Misili, kwizamtambikila Mulungu muna mulima uno."

13 Musa kamulongela Mulungu, "One nihahita kwa wanhu wa Isilaili na kuwalongela, 'Mulungu wa wasaho zenu kanhuma kumwenu,' nawo wezaniuza, 'Zina jake nani?' Niwalongeleze?"

14 Mulungu kamulongela Musa, "NIYE IYO NIYE." Na kalonga, "Walongele vino wanhu wa Isilaili, 'Ija iwomtanga IYO NIYE kanhuma kumwenu.' "

15 Iviya Mulungu kamulongela Musa, "Walongele Waisilaili, 'Mndewa Mulungu, Mulungu wa wasaho zenu na Mulungu wa Bulahimu na Mulungu wa Isaka na Mulungu wa Yakobo, kanhuma kumwenu.' Dino ijo zina jangu siku zose,

dizakumbukigwa kwa welesi wose.” 16 Hita
na ukawating'hanize hamwe walala wa Isilaili
na uwalongele, Mndewa Mulungu, Mulungu wa
wasaho zenu na Mulungu wa Bulahimu na wa
Isaka na wa Yakobo, kanilawilila na kanilongela,
“Niyawona yaja yomutendeligwa uko Misili.”

17 Na nimulaganilani kuwa nizamulavani muna
yamanhesa yenu uko Misili na kuwengiza muna
iisi ya Wakanaani na Wahiti na Waamoli na
Wapelizi na Wahivi na Wayebusi, isi ili na ulongo
unogile.

18 “Walala wa Isilaili wezakutegeleza,
maabaho weye na walala wa Isilaili mwizahita
kwa mfalume wa Misili na kumulongela,
‘Mndewa Mulungu, Mulungu wa Waebulaniya,
kaiting'hana na cheye. Lelo chokulamba
chilekelele chigende muna ichuwala siku nhatu
muladi chikamulavile nhambiko Mulungu
wetu.’ 19 Novimanya kuwa mfalume wa Misili
hezawalekela muhite mbaka yahavimanya
kuwa niye nina nguvu kufosa yeye. 20 Mbali
nizasang'hanila nguvu zangu kuwatagusa
Wamisili kwa kutenda vinhu va mauzauza haja.
Hamwande kezamulekelani muhite.

21 “Nizawatenda Wamisili wanoge kumwenu
muladi vondamusegele, sekemusegele makono
muhala. 22 Chila mwanamke wa Chiisilaili kezam-
pula mkaya miyage na ija yokala nayo muna ikaye
yake yamwing'he via va hela na via va zahabu
hamwe na mawalo. Mwizawavaza wanenu wa
chike na wa chilume. Vino niivo vondamusole
vinhu va Wamisili.”

# 4

### *Mulungu komwing'ha Musa udahi wa kutenda mauzauza*

1 Maabaho Musa kamwidika Mndewa Mulungu, “Mbali Waisilaili hawezanihuwila na hawezanitegeleza, mana wezalonga, ‘Mndewa Mulungu hakulawilile bule.’ ”

2 Mndewa Mulungu kamuuza Musa, “Icho choni chiwamhile mumkono wako?”

Musa kamwidika “Balati.”

3 Mndewa Mulungu kamulongela, “Ilagaze
hasi.” Ivo kailagaza hasi na igaluka iwa zoka.
Musa kakimbila. 4 Maabaho Mndewa Mulungu
kamulongela Musa, “Golosa mkono wako ujamhe
umkila.” Ivo kagolosa mkono wake kajamha,
na digaluka mhome kaidi muna umkono wake.
5 Mndewa Mulungu kamulongela, “Kwa kutenda
vino Waisilaili wezahuwila kuwa Mndewa
Mulungu, Mulungu wa wasaho zawo na Mulungu
wa Bulahimu na Mulungu wa Isaka na Mulungu
wa Yakobo, kakulawilila.”

6 Mndewa Mulungu kamulongela Musa
mwanza wekaidi, “Ika mkono mudiwalo
jako.” Musa keka mkono wake muna diwalo,
viyaulavile, ugaluka mzelu fana munhu yeli na
utamu wa mbende. 7 Maabaho Mndewa Mulungu
kamulongela, “Ika mkono wako muna diwalo
kaidi.” Katenda ivo, viyaulavile, ukala mgima,
fana mbende yake imwenga.

8 Maabaho Mndewa Mulungu kamulongela, “One hawakuhuwile hebu kutogola chilaguso

cha mauzauza cha mwanduso, yodahika chila-
guso cha mauzauza chino chekaidi wezachito-
gola. 9 Mbali one hawahuwile vilaguso vino
vidi hebu kukutegeleza, sola mazi kulawa muul-
wanda lwa Naili na yetile muna iisi inyalile, mazi
yondauyadehe kulawa muulwanda yezagaluka
damu muna iisi."

10 Musa kamulongela Mndewa Mulungu,
"Nokulamba Mndewa, niye sidaha kulonga
goya kwandusila mwaka, hata kusongela baho
viulongile na niye msang'hani wako, kwaviya
niye sidaha kulonga goya, na lulimi lwangu
luzama."

11 Mndewa Mulungu kamulongela, "Yelihi
yaumbile mulomo wa munhu? Hebu yelihi
yomtenda munhu yawe chibubu hebu
msuwamagutwi? Yelihi yomtenda munhu yalole
hebu yawe chipofu? Vino siyo niye Mndewa
Mulungu? 12 Lelo hita, nizakutaza kulonga na
kukufunza mbuli za kulonga."

13 Mbali Musa kamwidika, "Mndewa, nolamba
umtume munhu imwenga."

14 Ludoko lwa Mndewa Mulungu lumwakila
Musa na kalonga, "Vino kahabule sekulu wako
Haluni, ija Imulawi? Nivimanya kuwa yeye
kodaha kulonga vinogile. Kweli, kokwiza
kuiting'hana na weye na vondayakuwone
kezadeng'helela. 15 Weye kwizalonga
nayo na kumulongela yose yondayalonge,
niye nizawatazeni na kuwafunza mbuli
zondamutende. 16 Haluni kezakuwa mulonzi
wako na kezawalongela wanhu kwa ichimu
chako. Weye kwizakuwa fana mulungu

kumwake. 17 Sola balati dino muna umkono wako
muladi udahe kutenda vilaguso va mauzauza."

### *Musa kobwela Misili*

18 Maabaho Musa kabwela kaidi kwa Yesilo,
mkoi wake, na kumulongela. "Nokulamba
nilekelele nibwele kwa ndugu zangu uko Misili
nikawalole fana wang'hali wagima." Yesilo
kamulongela Musa, "Hita kwa tindiwalo."
19 Lusita Musa viyakalile uko Midiani, Mndewa
Mulungu kamulongela, "Bwela Misili, mana waja
wose wowalondile kukukoma wadanganika."
20 Musa kamsola muke wake na wanage,
kawakweza muna ichihongwe na kubwela Misili.
Kasola mhome ija Mulungu yoyamulongele
yaisole.
21 Kaidi Mndewa Mulungu kamulongela
Musa, "Vondaufike Misili utende haulongozi
ha mfalume wa Misili mauzauza yose
yonikwing'hile udahi wa kuyatenda. Mbali niye
nizautenda moyo wa mfalume wa Misili kuwa
mdala, nayo hezawalekela Waisilaili wasegele.
22 Maabaho kolondeka umulongele mfalume
wa Misili, Mndewa Mulungu kolonga, 'Isilaili ni
mwanangu chaudele. 23 Nikulongela umulekele
mwanangu yahite, muladi yanitambikile, mbali
kulema kumulekela yahite, ivo nizamkoma
chaudele wako wa chilume.' "
24 "Ikala viwakalile hanhu ha lago mwiinzila
kuhita Misili, Mndewa Mulungu kaiting'hana
nayo na kageza kumkoma. 25 Maabaho Sipola
muke wake, kasola dibwe dikutwa kakanha govi
da mwanage, na kumdalisa najo Musa mumgulu
na kalonga, 'Weye kwa mulume wa damu yangu.'

” 26 Kwa ichimu chino cha mwingizo, Sipola
kamulongela Musa, “Weye kwa mulume wa damu
yangu.” Kwa ivo Mndewa Mulungu kaulekela
ugima wa Musa.
27 Mndewa Mulungu kamulongela Haluni,
“Hita kuna ichuwala ukaiting'hane na Musa.”
Ivo Haluni kahita na waiting'hana kuna mulima
wa Mulungu, kamnonela. 28 Maabaho Musa
kamulongela Haluni chila chinhu chiyatumigwe
na Mulungu kulonga, iviya vilaguso va mauzauza
viyamulagilize yatende. 29 Musa na Haluni
wahita Misili na wawaduganya hamwe walala
wose wa Isilaili. 30 Haluni kawalongela chila
chinhu Mndewa Mulungu choyamulongele Musa.
Iviya katenda vilaguso haulongozi ha wanhu,
31 nawo wahuwila. Viwahulike kuwa Mndewa
Mulungu kawezila wanhu wa Isilaili kuwalola
viya viwoigaza chiusede, watumbala mavindi na
wamtosela Mulungu.

# 5

*Musa na Haluni haulongozi ha mfalume wa Misili*

1 Maabaho Musa na Haluni wahita kwa
mfalume wa Misili na kumulongela, “Mndewa
Mulungu, Mulungu wa Isilaili, kalonga,
‘Walekelele wanhu wangu wahite, muladi
wakanitendele dugila kuichuwala.’ ”
2 Mfalume wa Misili kawalongela, “Mndewa
Mulungu iyo yelihi mbaka nimtegeleze na
kuwalekelela Waisilaili wahite? Simmanyile bule
Mndewa Mulungu, na siwalekelela bule Waisilaili
wahite.”

3 Musa na Haluni wamwidika, “Mulungu wa
Waebulaniya kachilawilila yeye mwenyewo.
Lelo chilekele chigende mwanza wa siku nhatu
kuichuwala, chikamulavile nhambiko Mndewa
Mulungu, Mulungu wetu. One hachitendile ivo,
kezachikoma kwa matamu hebu ng'hondo.”
4 Mbali mfalume wa Misili kawalongela, “Mw-
eye Musa na Haluni, habali mowalekeza wanhu
sang'hano zawo? Mweye watumwa wose hiteni
kuna zisang'hano zenu! 5 Maabaho mfalume wa
Misili kawalongela, ‘Loleni, lelo wanhu wa isi
ni wengi kufosa Wamisili. Molonda kuwalekeza
sang'hano zawo!’ ”
6 Siku iyo iyo mfalume wa Misili kawalagiliza
wemilizi wa Chimisili na wanyapala wa Chiisi-
laili, kalonga, 7 “Sekemuweng'he wanhu wano
mayani ya kutendela matafali fana vimutendaga.
Walekeni wahite wakazahile wenyewo. 8 Mbali
peta ya matafali iwe fana yaja yowakalile woten-
geneza mwanduso, wekileni iyo iyo na seke-
muwahunguzile hata chidogo. Kwaviya wawo ni
wabwa wolonga, ‘Chileke chihite chikamulavile
nhambiko Mulungu wetu!’ 9 Wongezeni wanhu
wano sang'hano ndala muladi wagaye na waleke
kuhulika mbuli za uvwizi.”
10 Wemilizi wa Chimisili na wanyapala wa
Chiisilaili wahita na kuwalongela Waisilaili,
“mfalume wa Misili kawalongela kuwa
hezaweng'ha mayani. 11 Hiteni wenyewo
mkazahile mayani hohose hondamudahe
kuyapata, mbali molondeka mutende matafali
ya peta ija ija.” 12 Ivo wanhu wapwililika isi yose
ya Misili wozahila mayani yasigale ya kutendela

matafali. 13 Wemilizi wawo waiyoha kulonga,
“Komelezeni sang'hano zenu zimutendaga
fana baho umwaka vimukalile mogaliligwa
mayani.” 14 Wemilizi wa Chimisili wawatowa
wanyapala wa Chiisilaili wowasaguligwe kulola
goya sang'hano wahita kwa mfalume wa Misili,
walonga, “Habali hamkomeleza sang'hano yenu
na kufikiza peta ya matafali ija ija fana ya
umwaka?”
15 Maabaho wemilizi wa Chiisilaili weza na ku-
mulilila mfalume wa Misili, “Habali kochitendela
vino cheye wasang'hani wako? 16 Haching'higwa
kaidi mayani yoyose, na kuno chowangilizigwa
kutenda matafali. Iviya cheye wasang'hani wako
chotowigwa, mbali wabanange wanhu wako.”
17 Mfalume wa Misili kalonga, “Mweye
mwa wabwa, mana hamulonda kusang'hana
usang'hano, lekamana munipula niwalekelele
muhite na kumulavila nhambiko Mndewa
Mulungu. 18 Lelo hiteni mkasang'hane
usang'hano, mana hamwizakwing'higwa mayani,
na molondeka kutenda matafali peta ija ija.”
19 Lelo wemilizi wa Waisilaili wawona kuwa
wa muna yamagayo, mana walongeligwa,
“Hamwizaihunguza peta ya matafali ya chila
siku.”
20 Viwasegele kwa mfalume wa Misili,
wawafika Musa na Haluni wowakalile
wowagozela. 21 Wawalongela Musa na Haluni,
“Mndewa Mulungu yamuloleni na kuhumiza,
kwaviya muchitenda cheye fana china mnung'ho
wihile haulongozi ha mfalume wa Misili na
wasang'hani wake, mweye muweng'ha chimu
cha kuchikoma.”

### *Musa kolongelela kwa Mndewa Mulungu*

22 Maabaho Musa kabwela kwa Mndewa Mu-
lungu na kumulongela, “Mndewa Mulungu, ha-
bali kuwatendela vihile wanhu wano? Habali
kunhuma? 23 Kwandusila vinihitile na kulonga
na mfalume wa Misili kwa zina jako, kawatendela
vihile wanhu wano na weye hutendile chochose
kuwakombola.”

# 6

1 Mbali Mndewa Mulungu kamulongela
Musa, “Sambi kwizawona chondanimtendele
mfalume wa Misili. Mana kwa shuluti yangu
kezawalekelela wanhu wangu, kwa shuluti
kezawawinga muna iisi yake.”

### *Mulungu komtanga Musa*

2 Mulungu kamulongela Musa, “Niye Mndewa
Mulungu. 3 Nimulawililila Bulahimu na Isaka
na Yakobo fana viya Mulungu yeli na udahi,
mbali zina jangu Mndewa Mulungu siditendile
dimanyike kumwawo. 4 Iviya nitenda nawo
lagano jangu kuwa nizaweng'ha isi ya Kanaani,
uko wezakala fana nyambenyambe. 5 Iviya
nihulika kulongelela kwa Waisilaili, waja
Wamisili wawashulutiza kusang'hana sang'hano
za chitumwa, ivo nikumbuka lagano jangu.
6 Uwalongele Waisilaili, ‘Niye Mndewa Mulungu!
Nizamulavani na kumulekelani kulawa muna
utumwa wa Wamisili. Nizawinula mkono
wangu wili na ludabwa kuwatagusa Wamisili na
nizamkombolani. 7 Nizawatendani kuwa wanhu
wangu, niye nizakuwa Mulungu wenu. Mweye
mwizanimanya kuwa niye Mndewa Mulungu,

Mulungu wenu yoniwalekelele kulawa kuna
uutumwa muna iisi ya Misili. [8] Nizamgalani
muna iisi ija yoniilahile kuweng'ha Bulahimu
na Isaka na Yakobo. Nizamwing'hani mweye
iwe yenu, niye iyo Mndewa Mulungu.' " [9] Musa
kawalongela Waisilaili mbuli ino, mbali wawo
hawamtegeleze kwaviya wakala wafa moyo kwa
ichimu cha utumwa.

[10] Maabaho Mndewa Mulungu kamulongela
Musa, [11] "Hita kwa mfalume wa Misili ukamu-
longele kuwa kolondeka kuwalekelela Waisilaili
wasegele muna iisi yake."

[12] Mbali Musa kamwidika Mndewa Mulungu,
"Lola, Waisilaili hawanitegeleze. Lelo mfalume
wa Misili kezanitegeleza? Niye sidaha kulonga
vinogile!" [13] Mndewa Mulungu kawalagiliza
Musa na Haluni, "Walongele Waisilaili na
mfalume wa Misili kuwa niwalagilizani mweye
kuwalava Waisilaili muna iisi ya Misili."

### *Lukolo lwa Musa na Haluni*

[14] Wano wawo walangulizi wa ng'holo. Lubeni,
chaudele wa Yakobo kakala na wana wane wa
chilume, Henoki na Palu na Heziloni na Kalimi.
Wawo wakala lukolo lwa Lubeni. [15] Simeoni
kakala na wana sita wa chilume, Yemueli na
Yamini na Ohadi na Yakini na Sohali na Shauli,
mwana wa mwanamke wa Chikanaani. Wawo
wakala wa kaye ya Simeoni. [16] Yano ni mazina
ya wana wa chilume wa Lawi na nyelesi zawo,
fana viili maandiko yawo, Gelishoni na Kohasi
na Melali. Lawi kakala miyaka gana na malongo
matatu na saba. [17] Wana wa chilume wa Gelishoni
wakala Libini na Shimei, nawo wakala na lukolo

lwawo. 18 Wana wa chilume wa Kohasi wakala
Amilamu na Ishali na Hebuloni na Uzieli. Kohati
kakala miyaka gana malongo matatu na nhatu.
19 Wana wa chilume wa Melali wakala Mali na
Mushi. Wano wawo mawasaho wa ng'holo za
Walawi fana viili maandiko yawo.

20 Amilamu kamsola Yokebedi lumbu wa tati
yake, nayo kamwelekela Haluni na Musa. Amu-
lamu kakala miyaka gana malongo matatu na
saba. 21 Wana wa chilume wa Ishali wakala Kola
na Nefegi na Zikili. 22 Wana wa chilume wa Uzieli
wakala Mishaeli na Elisafani na Sisili.

23 Haluni kamsola Elisheba mndele wa Ami-
nadabu, iviya kakalalumbu jake Nashoni, nayo
kamwelekela Nadabu na Abihu na Eleazali na
Isamali. 24 Wana wa chilume wa Kola wakala Asili
na Elikana na Abiasafu. Wawo wakala wasaho wa
ng'holo za Kola. 25 Eleazali, mwana wa chilume
wa Haluni, kamsola imwe wa wandele wa Putieli,
iyo kamwelekela Finehasi. Wano wakala wakulu
wa ng'holo za Lawi.

26 Wano ni Haluni na Musa waja Mndewa
Mulungu woyawalongele, “Walaveni wanhu wa
Isilaili muna iisi ya Misili, lukolo kwa lukolo.”
27 Musa na Haluni niiwawo wowamulongele
mfalume wa Misili yawalekelele Waisilaili
walawe muna iisi ya Misili.

*Mndewa Mulungu kowalagiliza Musa na Haluni*

28 Mndewa Mulungu viyalongile na Musa muna
iisi ya Misili, 29 kamulongela Musa, “Niye Mndewa
Mulungu. Mulongele mfalume wa Misili chila

chinhu chonikulongela.” 30 Mbali Musa kamulon-
gela Mndewa Mulungu, “Vino mfalume wa Misili
kezanitegeleza? Niye sidaha kulonga vinogile.”

# 7

1 Mndewa Mulungu kamulongela Musa, “Niku-
tenda weye uwe fana mulungu kwa mfalume
wa Misili, sekulu wako Haluni kezalonga mbuli
zako fana mulongaji wako. 2 Mulongele Haluni
chila chinhu chonikulagilize, nayo kezamulon-
gela mfalume wa Misili yawalekelele Waisilaili
wasegele muna iisi yake. 3 Nizautenda moyo
wa mfalume wa Misili uwe mdala, nizakongeza
vilaguso vangu na mauzauza yangu muna iisi ya
Misili, 4 mbali mfalume wa Misili hezakutegeleza
bule. Maabaho nizagolosa mkono wangu uli na
ludabwa na kuitagusa isi ya Misili na kuwalava
wanhu wangu wa Isilaili kwa kuwatagusa ng'hani
Wamisili. 5 Wamisili wezanimanya kuwa niye iyo
Mndewa Mulungu, lusita vondanilaguse udahi
wangu na kuwalava Waisilaili muna iisi ya Mis-
ili.”
6 Musa na Haluni watenda fana viya Mndewa
Mulungu viyawalagilize. 7 Lusita luja viwamulon-
gele mfalume wa Misili, Musa kakala na miyaka
malongo manane na Haluni kakala na miyaka
malongo manane na mitatu.

## *Mhome ya Haluni*

8 Mndewa Mulungu kawalongela Musa na
Haluni, 9 “Mfalume wa Misili yahalonga na
mweye, ‘Ilaguseni kwa kutenda mauzauza,’
maabaho mulongele Haluni, ‘Sola mhome yako

na ilagaze hasi haulongozi wa mfalume wa Misili,
nayo izagaluka kuwa zoka.' "

10 Musa na Haluni wahita kwa mfalume wa
Misili na kutenda fana viya Mndewa Mulungu
viyawalagilize. Haluni kadilagaza hasi balati jake
haulongozi ha mfalume wa Misili na wasang'hani
wake, najo digaluka kuwa zoka.

11 Maabaho mfalume wa Misili kawatanga
wanhu wake weli na ubala na wahawi wa Misili,
nawo watenda fana ivo kwa uhawi wawo. 12 Chila
munhu kadilagaza hasi balati jake, najo digaluka
kuwa zoka. Mbali balati da Haluni diimela
mibalati yawo. 13 Moyo wa mfalume wa Misili
ukala ung'hali mdala, halondile kuwategeleza,
fana Mndewa Mulungu viyalongile.

*Hulo da damu*

14 Maabaho Mndewa Mulungu kamulongela
Musa, "Moyo wa mfalume wa Misili mdala
ng'hani, kolema kuwalekelela wanhu wahite.
15 Ivo hita ukaiting'hane na mfalume wa Misili
imitondo lusita viyohita kuulwanda lwa Naili.
Mgozele muingema ya ulwanda. Sola mhome
yako ija yoigaluke kuwa zoka. 16 Maabaho
mulongele mfalume wa Misili, Mndewa
Mulungu, Mulungu wa Waebulaniya, kanhuma
kumwako. Kolonga, 'Walekelele wanhu wangu
wahite, muladi wakanitambikile kuichuwala.
Mbali mbaka sambi weye kolema kutegeleza.
17 Lekamana Mndewa Mulungu kolonga kuwa
kwa mbuli ino, kwizanimanya kuwa niye iyo
Mndewa Mulungu. Lola nizayatowa mazi yano
yeli muulwanda lwa Naili kwa mhome ino inili
nayo mumkono wangu, nayo yezagaluka kuwa

damu. 18 Somba weli muna ulwanda lwa Naili
wezakufa, lwanda lose lwizanung'ha vundo na
Wamisili wezakwihilwa kung'wa mazi ya lwanda
ulo.' ”
19 Mndewa Mulungu kamulongela Musa, “Mu-
longele Haluni yasole mhome yake na kwiigolosa
uchanyha ya mazi ya Misili na uchanyha ya
nyanda zose na makolongo yose na malamba yose
na mazimbu yose, nayo yezakuwa damu. Isi
yose izakuwa na damu, hata muna iviya vose
va mbawo na mabwe.” 20 Musa na Haluni wa-
tenda fana viya Mndewa Mulungu viyawalagilize.
Haluni kenula uchanyha mhome yake haulon-
gozi ha mfalume wa Misili na wasang'hani wake,
kayatowa mazi ya lwanda Naili, nayo yose ya-
galuka kuwa damu. 21 Somba weli muulwanda
wafa, ulwanda lunung'ha vundo, ivo Wamisili
wapotwa kuyang'wa mazi ya lwanda ulo. Isi
yose ya Misili imema damu. 22 Mbali wahawi
wa Misili watenda vinhu fana ivo kwa uhawi
wawo, ivo moyo wa mfalume wa Misili ukala
ung'hali mdala, na halondile kuwategeleza Musa
na Haluni, fana Mndewa Mulungu viyalongile.
23 Mfalume wa Misili kabwela ukaye yake, hata
yano yalawilile hayagesile bule. 24 Wamisili wose
wahimba mumgwazo wa lwanda lwa Naili mu-
ladi wapate mazi ya kung'wa, mana wapotwa
kung'wa mazi ya lwanda lwa Naili.
25 Zifosa siku saba Mndewa Mulungu viya-
galuse mazi ya lwanda lwa Naili.

# 8

*Hulo da mabula*

1 Maabaho Mndewa Mulungu kamulongela
Musa, “Hita kwa mfalume wa Misili na umu-
longele, Mndewa Mulungu kolonga, ‘Walekelele
wanhu wangu wahite wakanitambikile. 2 One
uhalema kuwaleka wahite, nizaitowa isi yako
yose kwa kugala mabula. 3 Lwanda lwa Naili
lwizamema mabula, nayo yezakwingila mbaka
muna ikaye yako na muna ichiheleto chako cha
kugona na muna dikomwa jako na muna zikaye
za wanhu wako na wasang'hani wako. Mabula
yayo yezakwingila muna ivivu venu na muna
iviya va kubulugila usage. 4 Mabula yezakudanda
weye na wanhu wako na wasang'hani wako.’
” 5 Mndewa Mulungu kamulongela Musa,
“Mulongele Haluni yagolose mkono wake na
mhome yake uchanyha ya nyanda na uchanyha
ya makolongo na mazimbu, mabula yezalawilila
na kwenela chila hanhu muna iisi ya Misili.”
6 Haluni kagolosa mkono wake muna yamazi
yose ya Misili, mabula yalawilila na yaigubika isi
yose ya Misili. 7 Mbali wahawi wa Misili watenda
vinhu fana ivo kwa uhawi wawo, iviya mabula
yeza yaigubika isi.

8 Mfalume wa Misili kawatanga Musa na
Haluni, kawalongela, “Mpuleni Mndewa
Mulungu yayasegeze mabula yano kumwangu na
kwa wanhu wangu, nizawalekelela wanhu wenu
wahite wakamtambikile Mndewa Mulungu.”

9 Musa kamulongela mfalume wa Misili,
“Vinoga! Nilongele lusita loulonda nikupulile
kwa Mulungu, niwapulile wanhu wako na
wasang'hani wako. Nizampula yayadanganize

mabula yano yeli muna zikaye zenu, yezasigala
muna ulwanda lwa Naili muhala.”
10 Mfalume wa Misili kamwidika, “Igolo.”

Musa kamwidika, “Nizatenda fana viulongile,
muladi uvimanye kuwa habule munhu yoyose
yalingile fana Mndewa Mulungu, Mulungu wetu.
11 Mabula yezasegela kumwako na muna zikaye
zako na muna zikaye za wasang'hani wako na
wanhu wako, yezasigala muna ulwanda lwa Naili
muhala.” 12 Maabaho Musa na Haluni wasegela
kwa mfalume wa Misili, Musa kampula Mndewa
Mulungu yamsegezele mfalume wa Misili mab-
ula yayo yoyamgalile. 13 Mndewa Mulungu ka-
tenda fana viya Musa viyapulile, mabula wafa
muna zikaye zawo na muna zimbuga zawo na
muna imigunda yawo. 14 Wamisili wayaduganya
mabula yayo vibugulu bugulu, isi yose inung'ha
vundo. 15 Mfalume wa Misili viyawone mabula
yafa, kawa na moyo mdala kaidi, hawategeleze
Musa na Haluni, fana Mndewa Mulungu viya-
longile.

### *Hulo da usawasawa*

16 Maabaho Mndewa Mulungu kamulongela
Musa, “Mulongele Haluni yadigolose balati jake
na kuyatowa matimbwisi, nayo yezagaluka kuwa
usawasawa muna iisi yose ya Misili.” 17 Nawo
watenda ivo, Haluni kagolosa balati jake na kay-
atowa yamatimbwisi, nayo yagaluka usawasawa
uwavamba wanhu na wanyama. Matimbwisi
yose muna iisi ya Misili yagaluka kuwa usawa-
sawa. 18 Wahawi kwa uhawi wawo wageza ku-
tenda matimbwisi yagaluke kuwa usawasawa,

mbali wapotwa. Usawasawa uwo uwavamba
wanhu na wanyama. 19 Wahawi waja wamulon-
gela mfalume wa Misili, “Sang'hano ino kaitenda
Mulungu!” Mbali mfalume wa Misili kagendelela
kuwa na moyo mdala, hawategeleze Musa na
Haluni, fana Mndewa Mulungu viyalongile.

### *Hulo da ng'honzi*

20 Mndewa Mulungu kamulongela Musa, “Igolo
wiidawe ng'hani uhite kwa mfalume wa Misili
lusita viyohita kuulwanda na umulongele kuwa
Mndewa Mulungu kolonga, ‘Uwaleke wanhu
wangu wahite wakanitosele.’ 21 One uhalema
kuwalekelela wahite, nizakugalila mabumbila ya
ng'honzi, weye na wasang'hani wako na wanhu
wako. Ng'honzi wawo wezakwingila muna
zikaye zenu, kaye zose za Wamisili zizamema
mabumbila ya ng'honzi, hata isi yose wanhu
haweli.”

22 “Mbali siku iyo nizaibagula isi ya Gosheni
iwokala wanhu wangu, muladi ng'honzi
sekewawe uko. Kwa kutenda ivo kwizavimanya
kuwa niye Mndewa Mulungu na muna iisi ino.
23 Nizawabagula wanhu wangu na wanhu wako.
Chilaguso chino cha mauzauza chizalawilila
igolo.” 24 Mndewa Mulungu katenda fana
viyalongile. Mabumbila makulu ya ng'honzi
yengila muna ikaye ya mfalume wa Misili na
muna zikaye za wasang'hani wake. Wanhu wose
wa isi iyo wagazigwa na ng'honzi wawo.

25 Maabaho mfalume wa Misili kawatanga
Musa na Haluni na kawalongela, “Hiteni
mukamtosele Mulungu wenu muna iisi ino.”

26 Musa kamwidika, “Havinogile kutenda ivo,
mana nhambiko zondachimtambikile Mndewa
Mulungu, Mulungu wetu, zizawatenda Wamisili
wehilwe. Vino Wamisili wahachiwona cholava
nhambiko zoziwehila wawo, hawezachitowa na
mabwe mbaka chidanganike? 27 Cholondeka chi-
gende mwanza wa siku nhatu muna ichuwala
chikamulavile nhambiko Mndewa Mulungu, Mu-
lungu wetu, fana viyachilagilize.”

28 Mfalume wa Misili kawalongela,
“Nizamulekani muhite mukamulavile nhambiko
Mndewa Mulungu, Mulungu wenu kuichuwala,
mbali sekemuhite kutali ng'hani. Iviya nipulileni
na niye.”

29 Musa kamwidika, “Sambi vonisegela,
nizampula Mndewa Mulungu muladi igolo
yayasegeze mabumbila yano ya ng'honzi
kumwako na kwa wasang'hani wako na kwa
wanhu wako. Mbali weye sekeuchivwizile kaidi
kwa kulema kuwaleka wanhu wahite kumulavila
nhambiko Mndewa Mulungu.”

30 Maabaho Musa kasegela kwa mfalume wa
Misili na kampula Mndewa Mulungu, 31 Mndewa
Mulungu katenda fana Musa viyampulile.
Kawasegeza ng'honzi wose kwa mfalume wa
Misili na kwa wasang'hani wake na kwa wanhu
wake, hasigale hata ng'honzi imwe. 32 Mbali hata
mwanza uno mfalume wa Misili kakala na moyo
mdala na hawalekile wanhu wasegele.

# 9

*Hulo da mitamu ya wanyama*

1 Maabaho Mndewa Mulungu kamulongela
Musa, “Hita kwa mfalume wa Misili na
umulongele kuwa Mndewa Mulungu, Mulungu
wa Waebulaniya kolonga, ‘Walekele wanhu
wangu wahite muladi wakanitosele. 2 One
uhalema kaidi kuwaleka wahite na uhagendelela
kuwamhilila, 3 nizagolosa mkono wangu na
kuwagalila wanyama wako mitamu, ng'ombe na
vihongwe na mhunda na ngamiya na ng'hondolo
na luti. 4 Na nizagola wanyama wa Waisilaili na
wanyama wa Wamisili muladi hata mnyama
imwe wa Waisilaili sekeyafe.’ ” 5 Mndewa
Mulungu keka lusita na kalonga, “Igolo Mndewa
Mulungu kezatenda mbuli ino muna iisi.”

6 Igolo yake Mndewa Mulungu katenda fana
viyalongile. Wanyama wose wa Wamisili wafa,
mbali wanyama wa Waisilaili hafile hata imwe.
7 Mfalume wa Misili kauza chiya chilawilile kwa
wanyama wa Waisilaili, kalongiligwa kuwa hab-
ule hata mnyama imwe yafile. Hata ivo mfalume
wa Misili kagendelela kuwa na moyo mdala,
hawalekele wanhu wahite.

### *Hulo da maihu*

8 Maabaho Mndewa Mulungu kawalongela
Musa na Haluni, “Soleni maganza ya maivu ya
tanuli, maabaho Musa yayapigise uchanyha
haulongozi ha mfalume wa Misili. 9 Maivu
yayo yezakuwa timbwisi sisili dondajenele
muna iisi yose ya Misili. Nayo yezagala
maihu yondayatumbuke na kuwa vilonda
kwa wanhu na wanyama chila hanhu muna
iisi ya Misili.” 10 Ivo wasola maivu ya tanuli

na wema haulongozi ha mfalume wa Misili,
Musa kayapigisa uchanyha, nayo yawa maihu
yotumbuka na kuwa vilonda kwa wanhu
na wanyama. 11 Wahawi wapotwa kwima
haulongozi ha Musa kwaviya wakala na maihu,
mana Wamisili wose wakala na maihu. 12 Mbali
Mndewa Mulungu kautenda moyo wa mfalume
wa Misili uwe mdala na hawategeleze Musa na
Haluni, fana Mndewa Mulungu viyamulongele
Musa.

### *Hulo da mvula ya mabwe*

13 Maabaho Mndewa Mulungu kamulongela
Musa, "Igolo wiidawe ng'hani uhite kwa mfalume
wa Misili na umulongele kuwa Mndewa Mulungu,
Mulungu wa Waebulaniya, kolonga, 'Walekele
wanhu wangu wahite muladi wakanitosele.
14 Mana lelo nogala mahulo yangu yose kumwako
na wasang'hani wako na wanhu wako, ivo
kwizavimanya kuwa habule yalingile fana
niye muna izisi zose. 15 Mana one nihakugalile
mitamu ihile weye na wanhu wako, muhawile
mudanganika mumala. 16 Mbali nikuleka uwe
mgima muladi kulagusa udahi wangu. Ivo
wanhu wa zisi zose wezavimanya kuwa niye
iyo yelihi. 17 Mbali ung'hali kowalagusa udugi
wanhu wangu na huwalekela wasegele. 18 Lelo,
igolo lusita fana luno, nizagala mvula ng'hulu ya
mabwe, iyo hainalawilila muna iisi ya Misili,
kwandusila mwanduso wake mbaka sambi.
19 Lelo lagiliza wanyama wako na chila chinhu
chili kumgunda vikigwe muna ikaye. Kwaviya
mvula ya mabwe izamtonyela chila munhu na
mnyama yeli kumgunda na mnyama yeli kunze

ya kaye, wose wezakufa.’ ” 20 Wasang'hani
wamwenga wa mfalume wa Misili wadumba
na watenda fana viyalongile Mndewa Mulungu.
Wawagala watumwa wawo na wanyama wawo
muna ikaye. 21 Mbali waja wayehule mbuli ya
Mndewa Mulungu, wawaleka watumwa wawo
na wanyama wawo kuna imigunda.

22 Maabaho Mndewa Mulungu kamulongela
Musa, “Golosa mkono wako kuulanga, muladi
mvula ya mabwe itonye chila hanhu muna iisi ya
Misili. Iwatonyele wanhu na wanyama na vose vi-
handigwe muna imigunda.” 23 Ivo Musa kagolosa
mhome yake kuulanga, Mndewa Mulungu ka-
gala mvula ya mabwe na mbumo, lumwemwe
lumweka muna iisi. Mndewa Mulungu ka-
gala mvula ya mabwe muna iisi yose ya Misili.
24 Mvula ng'hulu ya mabwe ikalile na lumwemwe,
iyo habule munhu yoyose muna iisi ya Misili yai-
wonile mvula ilingile ivo kwandusila mwanduso.
25 Mvula iyo ya mabwe ibemenda chila chinhu
chikalile muna imigunda na chila hanhu muna
iisi ya Misili, wanyama na wanhu. Mabwe ya
mvula iyo yabemenda mimeya yose na mibiki
kuna imigunda. 26 Muna iisi ya Gosheni muhala,
kowakalile Waisilaili, hakukalile na mvula ya
mabwe.

27 Mfalume wa Misili kawatuma wanhu
wakawatange Musa na Haluni na kawalongela.
“Mwanza uno nitenda uhasanyi, Mndewa
Mulungu kanoga, mbali niye na wanhu wangu
chibananga. 28 Mpuleni Mndewa Mulungu,
mana mibumo ino na mvula ya mabwe viiyoha
ng'hani. Niye nizamulekelani musegele na hebu

hamwizagendelela kukala hano.”
29 Musa kamulongela, “Lusita vondanilawe
muna dibululu, nizakwinula makono yangu
kuchanyha na kumpula Mndewa Mulungu.
Mibumo izaleka, hebu hakwizakuwa na mvula
ya mabwe kaidi, muladi uvimanye kuwa zisi zose
ni za Mndewa Mulungu. 30 Mbali novimanya
kuwa weye na wasang'hani wako hamumdumba
Mndewa Mulungu.”
31 Mkonge na chinhu chilingile fana magota ya
uwele vose vikala vibanangigwa, kwaviya uwele
ukala na masuke na mkonge ukala wokwalika.
32 Mbali ngano na vinhu vimwenga vilingile fana
ngano havibanangike, kwaviya vokalama kukangala.
33 Musa kasegela ukaye kwa mfalume wa Misili
na kahita kunze ya bululu, kenula makono
yake kwa Mndewa Mulungu, mibumo na mvula
ya mabwe vileka. Mvula haitonyile muna iisi.
34 Mbali mfalume wa Misili viyawonile mvula
na mvula ya mabwe na mibumo vileka, katenda
uhasanyi kaidi. Kawa na moyo mdala yeye na
wasang'hani wake. 35 Ivo moyo wa mfalume
wa Misili ukala mdala, hawalekile Waisilaili
wahite, fana Mndewa Mulungu viyalongile kufosela Musa.

# 10

### *Hulo da nzige*

1 Maabaho Mndewa Mulungu kamulongela
Musa, “Hita kwa mfalume wa Misili, mana
niutenda moyo wake na moyo wa wasang'hani
wake kuwa mdala muladi nidahe kutenda

vilaguso vangu kumwawo. 2 Nitenda vino
muladi muwasimulile wanenu na wazukulu
zenu, viya viniwatendile Wamisili kuwa
wabozi kwa kutenda mauzauza kumwawo,
ivo mwizavimanya kuwa niye iyo Mndewa
Mulungu.”

3 Ivo Musa na Haluni wahita kwa mfalume
wa Misili na wamulongela, “Mndewa Mulungu,
Mulungu wa Waebulaniya, kolonga, ‘Vino
kwizalema kuinyendanyenda haulongozi wangu
mbaka zuwaki? Walekelele wanhu wangu
wahite, muladi wakanitosele. 4 One uhalema
kuwalekela wanhu wangu wasegele, igolo
nizagala nzige muna iisi yako. 5 Wezatanda
isi yose, habule munhu yondayadahe kuwona
hasi. Wezakuja vinhu visigale viifosile mvula ya
mabwe, hamwe na chila mbiki woukwima muna
imigunda yako. 6 Nzige wawo wezamema muna
zikaye zako na muna zikaye za wasang'hani wako
na muna zikaye za Wamisili wose. Wezakuwa
wengi ng'hani hata wasaho zenu hawanawawona
kwandusila viwelekigwe mbaka diyelo.’ ”
Maabaho Musa kahinduka na kasegela kwa
mfalume wa Misili.

7 Wasang'hani wa mfalume wa Misili wamu-
longela, “Vino ino kezachigaza mbaka zuwaki?
Waleke wanhu wano wahite muladi wakamtosele
Mndewa Mulungu, Mulungu wawo. Vino hugesa
kuwa isi ya Misili yodanganizigwa?”

8 Maabaho Musa na Haluni wagaligwa kaidi
kwa mfalume wa Misili, nayo kawalongela,
“Hiteni mukamtosele Mndewa Mulungu,
Mulungu wenu. Mbali welihi wondawahite?”

9 Musa kamwidika, “Chizahita wose, wabwanga
na walala. Chizasegela hamwe na wanetu wa
chike na wa chilume, ng'hondolo wetu na luti na
ng'ombe, mana cholondeka chimtendele dugila
da hishima Mndewa Mulungu.”

10 Kwa kuwazeha mfalume wa Misili
kawalongela, “Mndewa Mulungu yawe hamwe
na mweye one nihamulekeleni muhite na
wanenu. Kweli muna lungilo dihile muna
imizoyo yenu. 11 Haidahika! Walume muhala
wawo wondawahite kumtosela Mndewa
Mulungu, mana mbuli ino iyo yomulondile
umwaka.” Maabaho Musa na Haluni
wawingigwa haulongozi ha mfalume wa Misili.

12 Mndewa Mulungu kamulongela Musa,
“Golosa mkono wako uchanyha ya isi ya Misili,
muladi nzige walawilile wengile na kuja mimeya
yose muna iisi na vinhu vose visigazigwe na
mvula ija ya mabwe.” 13 Musa kagolosa mhome
yake uchanyha ya isi ya Misili, Mndewa Mulungu
kagala beho kulu kulawa ulawilo wa zua, dibuma
muna iisi ya Misili misi yose na chilo chose.
Vikuchile, beho diya da ulawilo wa zuwa digala
nzige. 14 Nzige wawo wenela chila hanhu
muna iisi ya Misili, na wakala bumbila kulu
ng'hani hawanalawilila nzige fana wawo hebu
hawezalawilila kaidi. 15 Mana waigubika isi yose
ya Misili, mbaka isi iwa na ziza. Waja mimeya
yose na matunda yose yasigale chipindi chiya
cha mvula ya mabwe. Muna iisi yose ya Misili
habule hata yani dimwe disigale hebu mbiki
hebu mmeya kuna imigunda.

16 “Baho mfalume wa Misili kawatanga Musa na

Haluni himahima na kawalongela, 'Nimuhasanya
Mndewa Mulungu, Mulungu wenu, na mweye
iviya nimuhasanyani. 17 Lelo nilekeleleni
uhasanyi wangu mwanza uno umwe muhala,
munipulile kwa Mndewa Mulungu, Mulungu
wenu, yanisegezele hulo dino dihile ng'hani.' ”
18 “Musa kasegela kwa mfalume wa Misili na
kampula Mndewa Mulungu. 19 Mndewa Mulungu
kagala beho da uswelo wa zuwa dili na nguvu
nyingi, ijo diwasegeza nzige waja na kuwagala
muna ibahali ya Shamu. Hasigale hata nzige
imwe muna iisi ya Misili. 20 Mbali Mndewa
Mulungu kautenda moyo wa mfalume wa Misili
kuwa mdala, hawalekelele Waisilaili wahite.”

### *Hulo da ziza*

21 Maabaho Mndewa Mulungu kamulongela
Musa, “Golosa mkono wako kuulanga, muladi
ziza totolo diigubike isi yose ya Misili. Ziza
dondadiwatende wanhu wababase.” 22 Lelo
Musa kagolosa mkono wake kuulanga, kukala
na ziza totolo muna iisi yose ya Misili kwa
siku nhatu. 23 Wanhu hawadahile kuiwona
hebu kusegela hanhu howakalile kwa siku nhatu.
Mbali Waisilaili wakala na bung'hulo uko Gosheni
kowakalile.
24 Mfalume wa Misili kamtanga Musa na kumulongela, “Hiteni mukamtosele Mndewa Mulungu,
hamwe na wanenu. Mbali ng'hondolo wenu na
luti na ng'ombe wolondeka wasigale hano.”
25 Mbali Musa kamwidika, “Uching'he
wanyama muladi chikamtimbulile Mndewa
Mulungu, Mulungu wetu. 26 Iviya wanyama
wetu wofugigwa cholondeka chisegele

nawo, hezasigala hata mnyama imwe hebu
mapaga, mana chizamtimbulila Mndewa
Mulungu mnyama kulawa muna iwanyama
wetu. Cheye hachivimanyile mnyama ilihi
yondachimtimbulile Mndewa Mulungu mbaka
vondachifike uko.”
27 Mndewa Mulungu kautenda moyo wa
mfalume wa Misili kuwa mdala, hawalekile
Waisilaili wahite. 28 Mfalume wa Misili
kamulongela Musa, “Segela haulongozi wangu!
Sekewize kuniwona kaidi. Mana siku yondawize
kaidi haulongozi wangu, kwizadanganika!”
29 Musa kamwidika, “Fana viulongile, sizakwiza
kukuwona kaidi.”

# 11

*Kukomigwa kwa welekwa wa udele*

1 Mndewa Mulungu kamulongela Musa, “Niza-
gala hulo dimwenga dimwe kwa mfalume wa
Misili na wanhu wake. Maabaho kezamulekani
musegele, na vondayamulekeni musegele, keza-
muwingani ng'hani. 2 Walongele Waisilaili kuwa
chila imwe wawo, muke kwa mulume, kolon-
deka yampule mkaya miyage via va hela na za-
habu.” 3 Mndewa Mulungu kawatenda Waisi-
laili wanogelwe na Wamisili. Iviya Musa kakala
munhu yohishimika ng'hani muna iisi ya Mis-
ili, na haulongozi ha mfalume wa Misili na
wasang'hani wake.
4 Ivo Musa kalonga, “Mndewa Mulungu ko-
longa, ‘Ichilo chikulu nizafosela Misili. 5 Chila
mwana chaudele wa chilume muna iisi ya Mis-
ili kezadanganika, kwandusila mwana chaudele

wa mfalume wa Misili yoyokala muna ichigoda
cha chifalume yeli muhazi wake, mbaka mwana
chaudele wa msang'hani wake wa chike yo-
dunda mhule muna idibwe. Hata wana chaudele
wa wanyama wofugigwa, nawo wose wezadan-
ganika. 6 Muna iisi yose ya Misili mwizakuwa
na ndilo ng'hulu, ndilo yake hainalawilila hebu
haizalawilila kaidi. 7 Mbali mwa Waisilaili kwiza-
kuwa kwabule ndilo na kwizakuwa na tindiwalo,
baho wezavimanya kuwa Mndewa Mulungu ni-
iyo yowabagula Wamisili na Waisilaili.' " 8 Musa
kakomelezela kwa kumulongela mfalume wa
Misili, "Wasang'hani wako wano wose wezanizila
na kuinama kwa hishima haulongozi wangu,
wezanilamba nisegele muna iisi ya Misili, niye na
wanhu wose wowonisondelela. Yahakomelezeka
yayo, nizasegela." Maabaho Musa kuno kana
ludoko kasegela kwa mfalume wa Misili.
9 Mndewa Mulungu kamulongela Musa,
"mfalume wa Misili hezakutegeleza, muladi
mauzauza yangu yongezeke muna iisi ya Misili."
10 Musa na Haluni watenda mauzauza yano yose
haulongozi ha mfalume wa Misili, mbali Mndewa
Mulungu kautenda moyo wa mfalume wa Misili
kuwa mdala. Hawalekile Waisilaili wasegele
muna iisi yake.

# 12

*Pasaka*

1 Mndewa Mulungu kawalongela Musa na
Haluni muna iisi ya Misili, 2 "Mwezi uno
wizakuwa mwezi wa mwanduso wa mwaka
kumwenu. 3 Walongele wanhu wose wa Isilaili

kuwa muna isiku ya longo ya mwezi uno, chila
munhu kolondeka yasole mwanang'hondolo
imwe, kwa chila kaye imwe. 4 Yahawa kaye ina
wanhu wadodo ng'hani, yolondeka kuilumba na
wanhu wa kaye ya mkaya miyage kuja inyama ya
kuwafaya wanhu wake, maabaho wezasagula
nyama chila munhu iyodaha kuja. 5 Sagula
bebelu kulawa mwa ng'hondolo hebu mwa
luti. Diwe da mwaka umwe na dilibule chilema
chochose. 6 Mwizamwika mbaka siku ya longo
na nne ya mwezi uno, maabaho Waisilaili wose
wezachinja wanyama wawo ichigulogulo nguku
zikwingila. 7 Wanhu wezasola damu ya mnyama
wawo na kuhaka mibiki yamhilile ulwivi lwa
ikaye yondawaje ng'hondolo. 8 Wezakuja nyama
ichilo icho vondawayoke, wezakuja hamwe na
gate hadigumigwe lusu na mboga zili usungu.
9 Sekemuje nyama mbisi hebu itogosigwe,
mbali yolondeka yokigwe yose, hamwe na
ditwi na migulu na nyama zake za mgati.
10 Sekemusigaze nyama yoyose mbaka imitondo,
one ihasigala mbaka imitondo, molondeka
muisome moto. 11 Vino ivo vondamuje nyama
iyo. Mwizakuwa mufunga mikwiji muna ivigudi
venu na muyawala vilatu na mwamha mhome
muna yamakono yenu kuisasala na mwanza,
kaidi mwizakuja himahima. Iyo ni *Pasaka ya
Mndewa Mulungu.

12 “Chilo icho nizafosela muna iisi ya Misili,
nizawakoma welekwa wa udele wose muna iisi ya
Misili, wanhu na wanyama. Nizaitagusa milungu

* **12:11** Pasaka fambulo jake “Kufosa uchanyha ya kaye.”

yose ya Misili. Niye iyo Mndewa Mulungu. 13 Lelo
damu ija izakuwa chilaguso chenu cha kulagusa
kaye zondamuwe. Niye vondaniwone damu iyo,
nizawafosani na hamwizapatigwa na dihile jojose
lusita vondaniwataguse Wamisili. 14 Siku ino iza-
kuwa ya lukumbuso kumwenu, mwizaitenda iwe
dugila kwa Mndewa Mulungu, hata nyelesi zenu
zose kwa lagilizo da siku zose kumwenu."

15 "Mndewa Mulungu kalonga, 'Kwa siku saba,
mwizakuja magate hayagumigwe lusu. Siku ya
mwanduso ya siku saba izo, mwizasegeza lusu
muna zikaye zenu. Munhu yoyose yahaja chinhu
chigumigwe lusu muna zisiku saba izo, kolondeka
yawingigwe na Waisilaili.' "

16 "Siku ya mwanduso na siku ya saba ni
mting'hano wa kutosa kwa Mndewa Mulungu,
mwizakuwa na dugila. Muna zisiku izo mbili
hamulondeka kusang'hana usang'hano wowose,
ila usang'hano wa kusasala ndiya. 17 Mwizatenda
dugila dino da magate hayagumigwe lusu fana
lukumbuso lwa siku vonimulavileni mweye
vibumbila va Waisilaili muna iisi ya Misili. Dugila
ijo dizatendigwa siku ino na nyelesi zenu zose
zikwiza fana lagilizo da siku zose. 18 Mwezi wa
mwanduso mwizakuja magate hayagumigwe
lusu, kwandusila ichigulogulo cha siku ya longo
na nne mbaka siku ya malongo maidi na imwe
ichigulogulo. 19 Muna zisiku izo saba, sekemuwe
na lusu jojose muna zikaye zenu. Munhu yoyose
yawe mfosanzila hebu mkaya, yahaja chinhu
chigumigwe lusu kezawingigwa na Waisilaili.
20 Hanhu hohose homukala, sekemuje chinhu

chigumigwe lusu. Molondeka muje magate hayagumigwe lusu.”

### *Pasaka ya mwanduso*

21 Musa kawatanga walala wose wa Waisilaili
na kuwalongela, “Chila imwe wenu yawasagulile
wanhu wa ng'holo zake mwanang'hondolo
wa chilume na kumchinja kwa ichimu cha
Pasaka. 22 Mwizasola mayani ya hisopo na
kuyachofa muna idamu mgati ya diziga na
kuihaka muna imibiki yamhilile ulwivi lwa
kaye zenu. Munhu yeyose sekeyalawe kunze
ya kaye ichilo icho mbaka imitondo. 23 Mana
Mndewa Mulungu kezafosa kuwakoma Wamisili,
one yahawona damu yoihakigwe muna imibiki
yamhilile ulwivi lwa kaye zenu, kezafosa. Wala
hezamuleka mdanganyi yengile muna zikaye
zenu na kumkomani. 24 Mweye mwizaika mbuli
ino kuwa lagilizo kumwenu na wanenu siku zose.
25 Vondamwingile muna iisi ija Mndewa Mulungu
yoyawalaganileni kumwing'hani, mwizatenda
dugila dino. 26 Wanenu vondawawauze, ‘Dugila
dino fambulo jake choni?’ 27 Mwizawedika, ‘Ino
ni nhambiko ya Mndewa Mulungu ya Pasaka,
kwaviya kafosa uchanyha ya kaye za Waisilaili
muna iisi ya Misili viyawakomile Wamisili, mbali
cheye hachikomile.’ ”

Maabaho Waisilaili waidulika matwi yawo na
kumtambikila Mndewa Mulungu. 28 Maabaho
Waisilaili wahita, watenda fana Mndewa Mu-
lungu viyawalagilize Musa na Haluni.

### *Zifa za wana chaudele wa Wamisili*

29 Chilo chikulu Mndewa Mulungu kawakoma
wana chaudele wa muna iisi ya Misili, kwandusila
chaudele wa mfalume wa Misili yoyakalile
muna ichigoda cha chifalume, mbaka chaudele
wa mfungwa na waudele wose wa wanyama.
30 Ichilo chiya, mfalume wa Misili na wasang'hani
wake na wanhu wose wa Misili, walamka.
Kukala na ndilo ng'hulu muna iisi yose ya
Misili, mana hakukalile na kaye hata imwe
munhu hadanganike. 31 Ichilo icho mfalume
wa Misili kawatanga Musa na Haluni na
kawalongela, "Lamkeni! Segeleni muna iwanhu
wangu. Segeleni mweye hamwe na Waisilaili
muladi mukamtosele Mndewa Mulungu, fana
vimulongile. 32 Soleni ng'hondolo wenu na luti
wenu na ng'ombe wenu, musegele. Na niye iviya
munitemele mate."
33 Wamisili wawahimiza Waisilaili wasegele
himahima kuna iisi yawo, walonga, "One
hamusegele, wose chizadanganika." 34 Ivo
Waisilaili wausola usage wawo haugumigwe lusu
na mahamha yawo ya kubulugila, waviguma
muna yamawalo yawo mmayega. 35 Waisilaili
watenda fana Musa viyawalongele, wawapula
Wamisili via va zahabu na hela na viwalo.
36 Mndewa Mulungu kamala kuwatenda
Waisilaili wanogelwe na Wamisili, Wamisili
waweng'ha Waisilaili chila chinhu chowapulile.
Vino niivo Waisilaili viwasolile vinhu va Wamisili.

## *Waisilaili wosegela Misili*

37 Waisilaili wasegela kulawa bululu da
Lamasesi wahita Sukosi. Wakala walume laki
sita, wanaake na wana hawapetigwe bule.

38 Wanhu wamwenga wengi wahita hamwe
nawo, ng'hondolo na luti na ng'ombe iviya wahita
hamwe nawo. 39 Kwaviya wakala wasegele
Misili himahima, hawadahile kusasala ndiya
ya kuja muna inzila, ila usage uja ubulugigwe bila
kugumigwa lusu, ivo woka magate hayagumigwe
lusu. 40 Waisilaili wakala Misili miyaka magana
mane na malongo matatu. 41 Viifikile siku
ya uhelelo ya mwaka wa magana mane na
malongo matatu, mabumbila yose ya wanhu
wa Mndewa Mulungu wasegela Misili. 42 Ikala
ichilo Mndewa Mulungu viyawakalize Waisilaili
muladi yawalave muna iisi ya Misili, chilo chino
yolondeka chikumbukigwe na Waisilaili wose
na nyelesi zawo, fana chilo cha hishima kwa
Mndewa Mulungu.

*Vihendo va Pasaka*

43 Mndewa Mulungu kawalongela Musa na
Haluni, "Malagilizo ya Pasaka ni yayo yano,
nyambenyambe yoyose hezakuja ndiya ya
Pasaka. 44 Mbali mtumwa yoyose yaguligwe,
yahengizigwa ulungwana kodaha kuja.
45 Nyambenyambe yofosa nzila hebu msang'hani
yolihigwa, halondeka kuja ndiya iyo.

46 "Ndiya yose yolondeka kudigwa muna ikaye
yoisasaligwe, sekemulawe nayo kunze hebu
sekemubene hata vuha dimwe da mnyama wa
Pasaka. 47 Wanhu wose wa Isilaili wolondeka
watende dugila ijo. 48 Nyambenyambe yoyose
yokala kumwenu yahalonda kutenda Dugila da
Pasaka da Mndewa Mulungu, teng'hu walume
wose wokala muna ikaye yake wolondeka

wengizigwe ulungwana, baho kezapeteka kuwa
mkaya na kutogoleligwa kutenda dugila. Mulume
yoyose hengizigwe ulungwana, sekeyaje ndiya ya
Pasaka. 49 Malagilizo yayo yayo yomsonhela
mkaya Muisilaili na nyambenyambe yokala
na mweye.” 50 Waisilaili wose watenda fana
Mndewa Mulungu viyawalagilize Musa na
Haluni. 51 Muna isiku iyo iyo Mndewa Mulungu
kawalava Waisilaili muna iisi ya Misili kwa
mabumbila.

# 13

### *Kusafyigwa kwa wana chaudele*

1 Mndewa Mulungu kamulongela Musa,
2 “Nisagulile wana chaudele wose wa chilume
wawe wangu, mana wa Waisilaili na wa
wanyama ni wangu.”

### *Dugila da Magate Hayagumigwe Lusu*

3 Musa kawalongela wanhu, “Mukumbuke siku
ino, siku yomusegezigwe muna iisi ya Misili, isi
yomukalile watumwa. Mana Mndewa Mulungu
kamulavani kwa udahi wake mkulu, muna isiku
ino sekemuje magate yagumigwe lusu. 4 Diyelo
muna umwezi wa Abibu, mwizasegela muna iisi
ya Misili. 5 Mndewa Mulungu vondayawagaleni
muna iisi ya Wakanaani na Wahiti na Waamoli
na Wahivi na Wayebusi, isi ija yoyawalahile
kuweng'ha wasaho zenu, isi ili na ulongo unogile.
Molondeka kuditenda dugila dino chila mwaka
muna umwezi uno. 6 Kwa siku saba muje magate
hayagumigwe lusu, muna isiku ya saba mwiza-
tenda dugila da hishima kwa Mndewa Mulungu.

7 Kwa siku saba hamulondeka kuja magate yagu-
migwe lusu. Magate yagumigwe lusu hebu lusu,
sekeviwoneke kumwenu na muna iisi yenu yose.
8 Na mwizawalongela wanenu siku ijo kuwa ni
kwa ichimu cha yoyawatendeleni Mndewa Mu-
lungu viyamulavileni muna iisi ya Misili. 9 Dugila
dino dizakuwa lukumbuso fana chilaguso muna
yamakono yenu hebu muna ivihanga venu, mu-
ladi siku zose chiwakumbuse kulonga malagilizo
ya Mndewa Mulungu. Mana Mndewa Mulungu
kamulavani muna iisi ya Misili kwa udahi wake
mkulu. 10 Ivo molondeka mutende dugila dino
lusita lwikigwe chila mwaka."

### *Waudele*

11 "Lusita Mndewa Mulungu vondayakugale
muna iisi ya Kanaani, kezamwing'hani fana
viyakulahile weye na wasaho zako, 12 kolondeka
kumwing'ha Mndewa Mulungu chila chaudele
wako wa chilume. Waudele wose wa chilume
wa wanyama wako wezakuwa wa Mndewa
Mulungu. 13 Mbali chaudele wa chihongwe
kwizamkombola kwa kuliha mwanang'hondolo,
mbali one hudaha kutenda ivo, kwizamkoma
kwa kumbena isingo yake. Iviya kwizamkombola
chila mwanago chaudele wa chilume.

14 "Hamwande mwanago yahakuuza fambulo
da chinhu chino, kwizamulongela, 'Mndewa
Mulungu kachilava muna iisi ya Misili kwa
udahi wake mkulu, kachisegeza muna iisi
ya Misili kochikalile watumwa. 15 Lusita
mfalume wa Misili viyakalile na moyo mdala
kalema kuchilekela chihite, Mndewa Mulungu
kawakoma chila chaudele wa chilume muna

iisi ya Misili, wanhu na wanyama. Lekamana
chomulavila nhambiko ya mnyama mulume
Mndewa Mulungu, mbali chowakombola
wanetu wa chilume. 16 Chino chizakuwa fana
chilaguso muna umkono wako na chilaguso
muna ichihanga chako, kuwa Mndewa Mulungu
kachilava muna iisi ya Misili kwa udahi wake
mkulu.' ”

*Kuloka ibahali*

17 Mfalume wa Misili viyawalekele wanhu
wahite, Mulungu halondile wafosele nzila ihitile
isi ya Wafilisiti, ingawa ikala nzila ikanhize.
Mulungu kalonga, "One kuhawa na ng'hondo,
wezadaha kugalula magesa yawo na kubwela
Misili." 18 Mbali Mulungu kawafoseza Waisilaili
kuna inzila nhali kufosela muichuwala, kuhita
bahali ya Shamu. Waisilaili wasegela Misili kuno
waisasala kwa ng'hondo.

19 Musa kaisola mivuha ya Yosefu, fana
viya Yosefu viyalagilize lusita yang'hali
hanadanganika. Kawalahiza Waisilaili, kalonga,
"Mulungu vondayamulaveni, molondeka
muipape mivuha yangu musegele nayo."
20 Waisilaili wasegela Sukosi na weka lago uko
Esamu muimhaka ya ichuwala. 21 Imisi Mndewa
Mulungu kawalongolela muna yamawingu
yalingile fana mhanda kuwalagusa nzila,
ichilo kawalongolela muna umoto ulingile
fana mhanda kuweng'ha bung'hulo, muladi
wadahe kugenda imisi na ichilo. 22 Mawingu
yalingile fana mhanda lusita lwa imisi na moto
ulingile fana mhanda lusita lwa ichilo, havilekile
kuwalongolela Waisilaili.

# 14

1 Maabaho Mndewa Mulungu kamulongela
Musa, 2 “Walongele Waisilaili wabwele hachisogo
na kwika mahema haulongozi ha Pihahilosi,
hagati ya Migidoli na Bahali ya Shamu,
haulongozi wa Baali Sefoni. 3 Mfalume wa
Misili kezagesa kuwa Waisilaili wowegela muna
iisi na chuwala chiwahindila. 4 Nizautenda
moyo wa mfalume wa Misili kuwa mdala, nayo
kezamsondelelani. Niye nizaipatila utunhizo kwa
kuwananga mfalume wa Misili na wakalizi wake,
Wamisili wezavimanya kuwa niye iyo Mndewa
Mulungu.” Maabaho Waisilaili watenda fana viya
viwalongeligwe.

5 Mfalume wa Misili viyalongiligwe kuwa
wanhu wamala kusegela, yeye na wasang'hani
wake wagalula magesa yawo na kulonga,
“Choni chino chochitendile? Chiwalekela
Waisilaili wasegele na chipuwa wasang'hani
wa kuchisang'hanila.” 6 Mfalume kasasala
mtuka wake wa kubululigwa na falasi na
kuwasola wakalizi wake. 7 Iviya kasola mituka
inogile magana sita na mituka imwenga yose
ya Wamisili, wakulu wa wakalizi wake wose,
wakwela mituka iyo. 8 Mndewa Mulungu
kautenda moyo wa mfalume wa Misili kuwa
mdala, muladi yawasondelele Waisilaili,
wowasegele kwa ugangamalo. 9 Wamisili hamwe
na falasi wawo wose na mituka yoibululigwa na
falasi na wakalizi wake wawasondelela Waisilaili,
wawafika wozenga lago hamgwazo ya bahali,
habehi na Pihahilosi, haulongozi wa Baali Sefoni.

10 Lusita Waisilaili viwamuwonile mfalume

wa Misili na wakalizi wake wowasondelela
wawo, wadumba ng'hani na kumulilila
Mndewa Mulungu yawataze. 11 Wamulongela
Musa, “Vino hakukalile na maleme muna
iisi ya Misili mbaka kuchigala chidanganikile
kuno kuchuwala? Habali kuchitendela yano
kwa kuchilava muna iisi ya Misili? 12 Vino
hachikulongele mbuli zino vichikalile ching'hali
muna iisi ya Misili? Chikulongela uchilekele
chigendelele kuwasang'hanila Wamisili. Ihawile
muhavu kuwasang'hanila Wamisili sembuse
kudanganikila kuno kuchuwala.”

13 Musa kawedika Waisilaili, “Sekemdumbe!
Imeni chigangamavu! Diyelo mwizawona viya
Mndewa Mulungu vondayawakomboleni. Mana
Wamisili wano womuwawona diyelo, hamwiza-
wawona kaidi. 14 Mndewa Mulungu kezawag-
ombeleni mweye, mweye molondeka munya-
male hupi.”

15 Mndewa Mulungu kamulongela Musa, “Ha-
bali monililila? Walongele Waisilaili wagendele
na mwanza. 16 Inula mhome yako na uigolose
uchanyha ya bahali uyagole yamazi, muladi
Waisilaili wadahe kufosa hagati ya bahali hanhu
hanyalile. 17 Niye nizawatenda Wamisili wawe
na mizoyo midala muladi wawasondeleleni mgati
muibahali, nizaipatila utunhizo kwa kumuhuma
mfalume wa Misili na wakalizi wake na mituka
yake na wakwela falasi wake. 18 Na wanhu wa isi
ya Misili wezanimanya kuwa niye Mndewa Mu-
lungu, vondaniipatile utunhizo kwa mfalume wa
Misili na mituka yake na wakwela falasi wake.”

19 Maabaho msenga wa Mulungu kawalon-

golela wakalizi wa Isilaili, kasegela na kukala
hachisogo chawo. Iiviya mhanda ija ng'hulu
ya wingu isegela na kukala hachisogo chawo,
20 ima hagati ya Wamisili na Waisilaili. Mhanda
ya wingu iyo ubanzi umwe ilava ziza, ubanzi
umwenga ilava bung'hulo. Ivo mabumbila yayo
maidi, wakalizi wa Misili na Waisilaili hawaik-
wenhukile chilo chose.

21 Musa kagolosa mkono wake uchanyha
muibahali, Mndewa Mulungu kaibweleza bahali
kuchisogo kwa beho kulu kulawa ulawilo wa
zuwa, beho ijo dibuma ichilo chose, diigola bahali
banzi mbili, hagati halawilila isi inyalile. Mazi
yaigola, 22 Waisilaili wafosa muibahali hana iisi
inyalile, mazi yaigola banzi mbili fana ng'huta.
23 Wamisili wawasondelela na wengila mgati
muna ibahali, falasi wawo wose na wakwela
falasi wawo na mituka yawo ya ng'hondo.
24 Habehi na kucha, Mndewa Mulungu kawalola
wakalizi wa Wamisili kulawa muna imhanda
ija ya moto na wingu, kawatenda bumbila da
wakalizi wa Misili wawe na lugano ng'hani.
25 Kayemiza maguludumu ya mituka yawo ya
ng'hondo, yakala yogenda ugaluga ng'hani.
Wamisili walonga, “Leka chiwakimbile Waisilaili!
Mndewa Mulungu kowagombela Waisilaili!”

26 Maabaho Mndewa Mulungu kamulongela
Musa, “Golosa mkono wako uchanyha ya bahali,
muladi mazi yabwele na kuwagubika Wamisili
na mituka yawo na wakwela falasi wawo.”
27 Musa kagolosa mkono wake uchanyha ya
bahali, vikukunguzuke mazi yabwela fana
viyakalile. Wamisili wageza kuyakimbila yamazi,

mbali Mndewa Mulungu kawasung'hila muna
yamazi. 28 Mazi yabwela na kugubika mituka
hamwe na wakwela falasi, wakalizi wose wa
mfalume wa Misili wowawasondelele Waisilaili
wadanganika muibahali. Hasigale Mmisili hata
imwe. 29 Mbali Waisilaili wafosa hagati ya bahali
hanhu hanyalile, mazi yakala fana ng'huta
kulume kwawo na kumoso kwawo.
30 Siku iyo Mndewa Mulungu kawakombola
Waisilaili kulawa muna yamakono ya Wamisili.
Waisilaili wawawona Wamisili mumgwazo mwa
ibahali wadanganika. 31 Waisilaili viwawonile
udahi mkulu Mndewa Mulungu uyalaguse kwa
Wamisili, Waisilaili wamdumba Mndewa Mulungu na wamuhuwila yeye na Musa msang'hani
wake.

# 15

*Wila wa Musa*

1 Maabaho Musa na Waisilaili wamwimbila Mndewa Mulungu wila uno, walonga,

“Nizamwimbila Mndewa Mulungu yeli uchanyha
ng'hani.
Kawasa muibahali falasi na wakwela falasi.
2 Mndewa Mulungu ni mgombezi wangu na
chimu cha wila wangu,
yeye iyo yonikombola.
Yeye ni Mulungu wangu, niye nizamtogoza,
Mulungu wa tati yangu, nizamtunhiza.
3 Mulungu ni galu wa ng'hondo,
Mndewa Mulungu niijo zina jake.

4 “Mituka ya mfalume wa Misili na wakalizi wake
kawasa muna ibahali,

wakalizi wake wanogile kufosa wose, wadumbukila muna ibahali ya Shamu.
5 Mazi mengi ya bahali yawagubika,
wadumbukila muibahali fana dibwe.
6 Mndewa Mulungu mkono wako wa kulume upata udahi mkulu,
Mndewa Mulungu, mkono wako wa kulume uwahonda wehi.
7 Kwa ukulu wako kowagwisa hasi wehi wako,
ludoko lwako lokwaka na kuwalunguza fana mabuwa yanyalile.
8 Kwa mhumuzi yako, mazi yaiduganya hamwe,
mawimbi yema zugaga fana ng'huta,
Mazi mengi ya hagati ya bahali yananahila.
9 Mwihi kalonga, 'Nizawawinza na kuwagwila,
nizagola utajili wawo na kusola vose vinilonda. Nizasomola ngugulila yangu, mkono wangu wizawadanganiza.'
10 Mbali kubuma kwa beho jako,
Wamisili wagubikigwa,
wadumbukila muna yamazi mengi fana dibwe.

11 "Mndewa Mulungu,
muna imilungu yelihi yalingile fana weye?
Yelihi yalingile fana weye uli na utunhizo ng'hani,
udumbiza kwa sang'hano za utunhizo?
12 Kugolosa mkono wako wa kulume,
na isi iwamela wehi wetu.

13 "Kwa ulondo wako wa kufunya umoyo, kuwalongoza wanhu wouwakombole,
kwa udahi wako mkulu kuwalongoza mbaka hanhu helile houkala.
14 Wanhu wa isi wahulika yayo na kugudemeka,

wanhu wokala Filisiti wengilwa na chinhu cha kudumbiza chiwagalile usungu.
15 Walangulizi wa Edomu wadumba,
walangulizi wa Moabu wagudemeka kwa kudumba,
wanhu wose wokala Kanaani mizoyo yawo imong'honyoka.
16 Wapatigwa na lugano na ludumbo.
Kwa ichimu cha ukulu wa nguvu zako,
wanyamala hupi fana dibwe.
Mbaka wanhu wako weye Mndewa Mulungu wafose,
mbaka vondawafose wanhu wako wouwakombole.
17 Kwizawengiza mgati na kuwemiza hana mulima wako,
hanhu haja houhasagule weye Mndewa Mulungu hawe hanhu handaukale,
hanhu helile houhazengile weye Mndewa Mulungu kwa mkono wako,
18 Mndewa Mulungu ni Mfalume siku zose."

### *Wila wa Miliamu*

19 Falasi wa mfalume wa Misili na mituka na wakwela falasi wake viwengile muibahali, Mndewa Mulungu kayabweleza mazi ya bahali na yawagubika. Mbali Waisilaili wagendelela kugenda hanhu hanyalile hagati ya bahali.

20 Mulotezi Miliamu, lumbu jake Haluni, kasola chigoma mumkono, na wanaake wose wamsondelela, watowa chigoma na wavina.
21 Miliamu kawembila,
"Mwimbileni Mndewa Mulungu yeli uchanyha ng'hani.

Kawasa muibahali falasi na wakwela falasi.”

### *Mazi yeli usungu*

22 Maabaho Musa kawalongoza Waisilaili
kulawa Bahali ya Shamu, wahita kuchuwala
cha Shuli. Siku nhatu wagenda muna ichuwala
bila kuyawona mazi. 23 Viwafikile hanhu
hatangigwe Mala, hawadahile kung'wa mazi
ya uko kwaviya yakala usungu. Lekamana hanhu
baho hatangigwa Mala. 24 Wanhu walongelela
kwa Musa, walonga, “Lelo chizakung'wa choni?”
25 Maabaho Musa kamulilila Mndewa Mulungu,
Mndewa Mulungu kamulagusila tambi da biki,
Musa kadivabika muna yamazi, mazi yose yahola.

Uko Mndewa Mulungu kaweng'ha Waisilaili
malagilizo na ndagilizi muladi yawageze,
26 kawalongela, “One muhaditegeleza vinogile
dizi jangu niye Mndewa Mulungu, Mulungu
wenu, na kutenda yaja yanogile haulongozi
wangu na kutegeleza ndagilizi na malagilizo
yangu, niye sizamgalileni matamu yaja
yoniwagalile Wamisili. Kwaviya niye iyo Mndewa
Mulungu yonimuhonyani.”

27 Maabaho wafika Elimu, kokukalile na nzasa
longo na mbili na mitende malongo saba. Uko
weka mahema jawo habehi na mazi.

# 16

### *Mana na ng'hwale*

1 Maabaho Waisilaili wose wasegela kulawa
Elimu na wahita kuna ichuwala cha Sini, chili
hagati ya Elimu na Sinai, muna isiku ya longo
na tano ya mwezi wekaidi, lusita viwasegele

muna iisi ya Misili. 2 Kuja kuichuwala Waisi-
laili wose walongelela kwa Musa na Haluni,
3 wanhu wa Isilaili wawalongela, “Muhavu Mn-
dewa Mulungu yahachikomile vichikalile muna
iisi ya Misili kochikalile chija nyama na magate
mbaka chiguta. Mbali mweye muchigala kuno
kuichuwala muladi muchikome chose na nzala.”
4 Mndewa Mulungu kamulongela Musa,
“Nizamtonyelani mvula ya magate kulawa
kuulanga. Chila siku wanhu wezalawa na
kuduganya ndiya ya siku iyo. Kwa nzila ino
nizawageza niwone fana wezasondelela ndagilizi
zangu hebu hawezasondelela. 5 Siku ya sita
vondawasasale ndiya yowaduganye, chiyasi icho
chizakuwa miyanza midi ya ndiya ya chila siku.”

6 Musa na Haluni wawalongela Waisilaili wose,
“Ichigulogulo mwizavimanya kuwa Mndewa
Mulungu iyo yamulavileni muna iisi ya Misili.
7 Imitondo mwizawona utunhizo wa Mndewa
Mulungu, kwaviya kahulika kulongelela kwenu
kwa Mndewa Mulungu. Vino cheye china
nani mbaka mudahe kulongelela kumwetu?”
8 Maabaho Musa kawalongela, “Ichigulogulo
Mndewa Mulungu kezamwing'hani nyama muje,
imitondo kezamwing'hani magate muje mwigute,
kwaviya kahulika kulongelela kwenu. Vino
cheye china nani mbaka mulongelele kumwetu?
Hamulongelele kumwetu mbali mulongelela kwa
Mndewa Mulungu.”

9 Maabaho Musa kamulongela Haluni, “Walon-
gele wanhu wose wa Isilaili wahite na kwima
haulongozi ha Mndewa Mulungu, mana kahu-
lika kulongelela kwenu.” 10 Haluni viyakalile

kolonga na Waisilaili wose, walola kuichuwala,
utunhizo wa Mndewa Mulungu ulawilila muna
diwingu. 11 Mndewa Mulungu kamulongela
Musa, 12 “Nihulika kulongelela kwa Waisilaili.
Walongele, ‘Nguku zikwingila wezakuja nyama
na imitondo wezakuja magate. Baho mwizav-
imanya kuwa niye iyo Mndewa Mulungu, Mu-
lungu wenu.’ ” 13 Ichigulogulo diza bumbila da
ng'hwale na wadigubika dilago da Waisilaili, imi-
tondo nhungwe izunguluka lago jose. 14 Nhungwe
viimalile, kuichuwala kuwa na chinhu chilingile
fana gate sisili. 15 Waisilaili viwawone chinhu
icho waiuza, “Chino choni?” Mana hawavimany-
ile chikala choni.

Musa kawalongela, “Dino ijo gate
doyamwing'hileni Mndewa Mulungu muje.
16 Chino icho chiyalagilize Mndewa Mulungu,
‘Chila munhu yaduganye ndiya kwa kaye yake
viyodaha kuja. Yamdondolele mhishi imwe
yoimfaya chila munhu yeli muna ikaye yake.’
”

17 Waisilaili watenda fana viwalongeligwe,
wamwenga waduganya nyingi na wamwenga
chidogo. 18 Na viwapimile mhishi ziwaduganye,
munhu yaduganye ndiya nyingi hapatile nyingi
ng'hani, munhu yaduganye chidogo hapatile
chidogo ng'hani. Chila munhu kaduganya ndiya
yoimfaya. 19 Maabaho Musa kawalongela,
“Munhu yoyose sekeyasigaze ndiya iyo mbaka
imitondo.” 20 Mbali wawo hawamtegeleze Musa,
ivo wasigaza ndiya mbaka imitondo. Mbali
imitondo ndiya iyo iwola, ilava mavunyo na
kunung'ha vundo. Ivo Musa kawawonela ludoko

ng'hani. [21] Chila imitondo wanhu woduganya
ndiya yoimfaya kuja. Zuwa vidikwelile na
kuwa kali, ndiya isigale hamgwazo ya nzila
ilumbuzuka.

[22] Siku yesita Waisilaili waduganya ndiya iyo
miyanza midi kufosa mwanduso, chila munhu
mhishi mbili. Ivo walangulizi wose wa Waisi-
laili wamuhitila Musa na wamulongela mbuli
izo. [23] Musa kawalongela, "Vino niivo viyalag-
ilize Mndewa Mulungu, 'Igolo ni siku ya kuhu-
mula, Siku ya Mhumulo yelile ya Mndewa Mu-
lungu. Ivo hiteni mukambike hebu mukakimuse
ndiya yomulonda diyelo, ndiya yondaisigale ikeni
mbaka igolo.' "

[24] Ivo weka goya indiya mbaka imitondo fana
Musa viyawalongele, nayo haiwolile na hailav-
ile mavunyo hebu hainung'hile vundo. [25] Musa
kawalongela, "Diyeni ndiya ino diyelo, kwaviya
diyelo ni Siku ya Mhumulo ya Mndewa Mu-
lungu. Diyelo hamwizafika ndiya yoyose kunze
ya lago. [26] Mwizaduganya ndiya kwa siku sita,
mbali muna isiku yesaba, Siku ya Mhumulo, hak-
wizakuwa na chinhu chochose."

[27] Siku ya saba wanhu wamwenga wahita
kudondola ndiya, mbali hawafikile chinhu.
[28] Maabaho Mndewa Mulungu kamuuza Musa,
"Mwizalema kwamha malagilizo yangu na
ndagilizi zangu mbaka zuwaki? [29] Kumbukeni
kuwa Mndewa Mulungu kamwing'hani Siku
ya Mhumulo, lekamana muna isiku yesita
komwing'hani magate kwa siku mbili. Muna
isiku yesaba, chila munhu nayakale hanhu hayeli.

Munhu yoyose sekeyalawe kunze siku yesaba.”
30 Ivo siku yesaba wanhu wahumula.

31 Waisilaili waitanga ndiya iyo “Mana.” Ikala
fana uhemba mzelu na mumulomo ilinga fana
gate sisili digumigwe uki. 32 Musa kawalon-
gela, “Vino ivo viyalagilize Mndewa Mulungu,
‘Soleni lita mbili za mana na mwiike kwa ichimu
cha nyelesi zikwiza, muladi wawone ndiya yon-
imulisileni kuichuwala chipindi chinimulavileni
muna iisi ya Misili.’ ”

33 Musa kamulongela Haluni, “Sola nongo uk-
agume lita mbili za mana, wiike haulongozi ha
Mndewa Mulungu ikalizigwe kwa ukalangama
kwa nyelesi zikwiza.” 34 Fana Mndewa Mulungu
viyamulagilize Musa, Haluni keka mana* hau-
longozi ha vibawo va mabwe va ukalangama,
muladi ikigwe goya. 35 Waisilaili waja mana
kwa miyaka malongo mane, mbaka viwafikile
muna iisi inogile kukala, isi ili muna imhaka ya
Kanaani. 36 Mhamba ya mana lita mbili ikala
chinhu chimwe muna ichila vinhu longo, ningo
iyo izoweleke yoitangigwa efa.

# 17

*Mazi kulawa muna uluwe*

1 Wanhu wose wa Isilaili walawa muna
ichuwala cha Sini, wandusa mwanza kulawa
hanhu hamwe kuhita hamwenga fana viya
Mndewa Mulungu viyawalagilize. Wazenga
lago uko Lefidimu, mbali hakukalile na mazi

* **16:34** Fambulo da zina dino “mana” dikala “chini ni choni?”

ya kung'wa. 2 Walongelela kwa Musa, walonga,
“Ching'he mazi ya kung'wa.”

Musa kawedika, “Habali molongelela kumwangu? Habali momgeza Mndewa Mulungu?”

3 Mbali wanhu wakala na ng'hilu ng'hani, walongelela kwa Musa, walonga, “Habali kuchilava kuna iisi ya Misili uchikome na ng'hilu cheye na wanetu na wanyama wetu?”

4 Musa kamulililila Mndewa Mulungu, kalonga, “Niwatendele choni wanhu wano? Habehi wezanitowa na mabwe.”

5 Mndewa Mulungu kamulongela Musa, “Fosa kuulongozi wa wanhu wano na uwasole walala wawo wamwenga. Iviya usole mhome ija youitowele lwanda lwa Naili na uhite.
6 Lola, nizakwima haulongozi wako muna uluwe uko Holebu. Utowe luwe ulo, mazi ya kung'wa wanhu yezalawa muna uluwe.” Musa katenda ivo haulongozi ha walala wa Isilaili.

7 Musa kahatanga hanhu baho Masa na Meliba, kwaviya Waisilaili walongelela na kumgeza Mndewa Mulungu, walonga, “Vino kweli Mndewa Mulungu kahamwe na cheye?”

### *Ng'hondo na Waamaleki*

8 Waamaleki weza na kuitowa na Waisilaili uko
Lefidimu. 9 Musa kamulongela Yoshua, “Sagula walume uhite ukaitowe na Waamaleki. Igolo nizakwima kuinhembeti ya mulima, noyamhilila mhome ija ya Mulungu muna umkono wangu.”

10 Ivo Yoshua kawatowa Waamaleki fana viya Musa viyamulagilize. Musa na Haluni na Huli
wahita kuinhembeti ya mulima. 11 Chila Musa

viyokwinula makono yake kuchanyha, Waisi-
laili wakala wohuma, viyohumulusa makono
yake, Waamaleki wakala wohuma. 12 Mbali
hamwande makono ya Musa yalegela. Ivo Haluni
na Huli wasola dibwe na wadika habehi na Musa,
nayo kakala. Maabaho wayamha na kwinula
mikono yake, imwe kenula mkono wa kulume
na imwenga mkono wa kumoso. Ivo makono ya
Musa yagendelela kugangamala kuno yenuligwa
uchanyha mbaka zuwa vidiswile. 13 Ivo Yoshua
kawahuma Waamaleki kwa upanga.

14 Maabaho Mndewa Mulungu kamulongela
Musa, "Yandika mbuli ino muna ichitabu,
maabaho igong'onde muna yamagutwi ya
Yoshua iwe lukumbuso kwaviya nizawasegeza
Waamaleki wose muna iisi yose." 15 Musa
kazenga lupango na kachitanga, "Mndewa
Mulungu kanitenda nihume." 16 Kalonga, "Mana
makono yenuligwa uchanyha kuna ichigoda
cha chifalume cha Mndewa Mulungu. Mndewa
Mulungu kezakuwa na ng'hondo na Waamaleki
siku zose."

# 18

### *Yesilo komulaula Musa*

1 Yesilo mkulu wa nhambiko wa Midiani yeli
mkoi wa Musa, kahulika chila chinhu Mndewa
Mulungu chiyamtendele Musa na Waisilaili, na
viya viyawalavile kuna iisi ya Misili. 2 Ivo Yesilo
keza kwa Musa, kamgala Sipola muke wa Musa,
Musa yoyamulekile kuchisogo, 3 hamwe na wan-
age waidi wa chilume wa Musa. Mwana wa

mwanduso katangigwa Gelishomu. Musa kam-
tanga zina dino kwaviya kalonga, “Niye nikala
nyambenyambe muna iisi ya ugeni.” 4 Wekaidi
katangigwa Eliezeli, kwaviya kalonga, “Mulungu
wa tati yangu kanitaza na kanikombola kulawa
muna upanga wa mfalume wa Misili.” 5 Yesilo
mkoi wa Musa, hamwe na muke wa Musa na
wanage, weza kwa Musa kuichuwala koyekile
lago habehi na mulima wa Mulungu. 6 Yesilo
katuma usenga kwa Musa, “Niye Yesilo mkoi
wako, nokwiza na muke wako na wanage waidi.”
7 Musa kalawa kunze kumuhokela Yesilo, kam-
tumbalila mavindi na kamnonela. Waiuzag-
iza mbuli za uhonyaji, maabaho wengila muna
dilago da Musa. 8 Musa kamulongela mkoi
wake chila chinhu Mndewa Mulungu chiyamten-
dele mfalume wa Misili kwa ichimu cha Waisi-
laili na kusonhela mbuli ndala zose ziwapatile
mnzila na viya Mndewa Mulungu viyawakom-
bole. 9 Yesilo kadeng'helela viyahulike mbuli
zose zinogile Mndewa Mulungu ziyawatendele
Waisilaili kwa ichimu cha kuwakombola muna
yamakono ya Wamisili. 10 Na kamulongela,
“Mtunhize Mndewa Mulungu, yoyawakomboleni
kulawa kwa mfalume wa Misili na Wamisili!
Yatunhizigwe Mndewa Mulungu, yoyawagom-
bole wanhu wake kulawa kuutumwa! 11 Lelo
nivimanya kuwa Mndewa Mulungu ni mkulu ku-
fosa milungu yose, mana kawakombola wanhu
wano muna yamakono ya Wamisili wowawaten-
dele magoda.” 12 Maabaho Yesilo mkoi wa Musa
kamulavila Mndewa Mulungu nhambiko za ku-
timbuligwa na nhambiko. Haluni keza na walala

wa Isilaili muladi waje ndiya hamwe na Yesilo
haulongozi ha Mulungu.

13 Igolo yake Musa kakala kowahumiza Waisi-
laili, nawo wema kuno wamzunguluka kulawa
imitondo mbaka ichigulogulo. 14 Yesilo mkoi wa
Musa viyawonile mbuli zose Musa ziyawatendele
Waisilaili, kamuuza, “Chino choni chouwatendela
wanhu? Habali kolamula nhaguso wiidumwe
kuno wanhu wano wose wakuzunguluka kulawa
imitondo mbaka ichigulogulo?”

15 Musa kamwidika, “Kwaviya wanhu wokwiza
kumwangu kuuza viyolonda Mulungu. 16 Wanhu
wahagomba wokwiza kumwangu na niye
nowahumiza na kuwalongela malagilizo na
ndagilizi za Mulungu.”

17 Maabaho Yesilo kamulongela Musa, “Viu-
sang'hana havinogile. 18 Weye na wanhu wano
mwizalegela, kwaviya sang'hano ino ndala. Hu-
daha kuisang'hana wiidumwe. 19 Lelo nitegeleze
niye na nizakulongela vinigesa, Mulungu yawe
hamwe na weye. Weye kwizahita haulongozi
ha Mulungu kwa ichimu cha wanhu na kum-
galila magayo yawo. 20 Kolondeka uwafundize
malagilizo na ndagilizi za Mulungu na kuwala-
gusa viya viwolondeka kukala na kusang'hana
usang'hano. 21 Mbali kwa mbuli zimwenga sag-
ula walume weli na udahi mwa iwanhu wose.
Wanhu womdumba Mulungu na wanhu goya
na hawalonda kusola chochose muladi kubena
malagilizo, weng'he usang'hano wa kuwemiliza
wanhu muna yamabumbila ya wanhu elufu na
mabumbila ya wanhu gana na mabumbila ya
wanhu malongo matano na mabumbila ya wanhu

longo. 22 Wawo wezakuwa na malundo chila
siku kuhumiza mbuli za wanhu. Mbuli ndala
wezakugalila weye, mbali mbuli ndodondodo
wezazilamula wenyewo. Kwa nzila iyo kwiz-
adaha kuitenda sang'hano yako ihuhe, kwaviya
wanhu wezailumba na weye muna isang'hano
iyo. 23 Uhatenda ivo na ihawa niivo viyolonda
Mulungu, kodaha kufunya umoyo, wanhu wano
wose wezadaha kubwela kumwawo kwa tindi-
walo."

24 Musa kamtegeleza mkoi wake na katenda
fana viyamulongele. 25 Musa kasagula wanhu
walume weli na udahi mwa Waisilaili, kawatenda
kuwa walangulizi wa mabumbila ya wanhu elufu
na mabumbila ya wanhu gana na mabumbila
ya wanhu malongo matano na mabumbila ya
wanhu longo. 26 Wasang'hana fana wasemi wa
wanhu lusita lose. Mbuli zizamile wamgalila
Musa, mbali mbuli ndodondodo wazikomeleza
wawo wenyewo. 27 Maabaho Musa na Yesilo mkoi
wake wailaga, nayo Yesilo kabwela kuna iisi yake.

# 19

*Waisilaili kuna mulima wa Sinai*

1 Siku ya mwanduso ya mwezi wetatu Waisi-
laili viwalawile muna iisi ya Misili, wafika kuna
ichuwala cha Sinai. 2 Viwasegele Lefidimu na
kufika kuichuwala cha Sinai, Waisilaili wazenga
lago haulongozi wa mulima wa Sinai. 3 Maabaho
Musa kakwela kumulima kwa Mulungu. Mndewa
Mulungu kamtanga Musa kulawa kuna mulima,
kamulongela, "Vino niivo vondauwalongele we-
lesi wa Yakobo na Waisilaili. 4 'Mweye wenyewo

muwona viniwatendile Wamisili na viya vinim-
solileni fana masumula viyosola wanage kwa
mabawa yake, nimgalani kumwangu. 5 Lelo, one
mwahanitegeleza na kudika goya lagano jangu,
mwizakuwa wanhu wangu mwa makabila yose,
mana isi yose yangu. 6 Mweye kumwangu mwiz-
akuwa ufalume wa wakulu wa nhambiko na
wanhu welile.' Zino niizo mbuli zondauwalon-
gele Waisilaili."

7 Ivo Musa kahumuluka na kawatanga hamwe
walala wa Waisilaili, kawalongela chila chinhu
Mndewa Mulungu chiyamulagilize. 8 Maabaho
wanhu wose wedika hamwe, walonga, "Chiza-
tenda chila chinhu chiyalongile Mndewa Mu-
lungu." Ivo Musa kamulongela Mndewa Mulungu
chiwalongile wanhu wawo.

9 Mndewa Mulungu kamulongela Musa, "Niza-
kwiza muna diwingu dizamile, muladi wanhu
wahulike vinilonga na weye na wezakuhuwila
siku zose.

"Musa kamulongela Mndewa Mulungu chiwa-
longile wanhu wawo." 10 Mndewa Mulungu ka-
mulongela Musa, "Hita kwa wanhu ukawalongele
waisafye diyelo na igolo. Wolondeka wayasunhe
mawalo yawo 11 na waisasale kwa chisindo, mana
siku iyo yetatu niye Mndewa Mulungu nizahumu-
luka kulawa uchanyha ya mulima wa Sinai hau-
longozi ha wanhu wose. 12 Wekile mhaka wanhu
kuzunguluka mulima. Walongele, 'Muiteganye
sekemukwele kumulima hebu kubojoga mhaka
yake. Munhu yoyose yondayaudalise mulima
kezadanganika.' 13 Munhu yoyose yondayadalise
mulima, kolondeka yatowigwe na mabwe hebu

msale, munhu hebu mnyama, kezadanganika.
Mbali mhalati vondailile, wanhu wezakwela ku-
mulima.”
14 Musa viyahumuluke kuna mulima,
kawahitila wanhu na kawasafya, nawo
wayasunha mawalo yawo. 15 Maabaho Musa
kawalongela wanhu, “Muisasale kwa chisindo,
mulume yoyose sekeyambandame muke wake.”

16 Siku yetatu imitondo uchanyha ya mulima
kulawilila mibumo na mimwemwe na wingu
dizamile. Iviya dihulikika dizi da mhalati
dodiwagudemeze wanhu wose wa kuna dilago.
17 Maabaho Musa kawalava wanhu mudilago
na kawagala wakaiting'hane na Mulungu,
wema hasi ya mulima. 18 Mulima wa Sinai
wakala wogubikigwa na yosi, kwaviya Mndewa
Mulungu kahulumuka muna umoto. Yosi
dikwela uchanyha fana yosi da tanuli, mulima
wose wagudemeka ng'hani. 19 Dizi da mhalati
digendelela kulanduka. Musa kalonga na
Mulungu, Mulungu nayo kamwidika muna
umbumo. 20 Mndewa Mulungu kahumuluka
kuinhembeti ya mulima wa Sinai na kamtanga
Musa kuna inhembeti. Ivo Musa kakwela kuna
inhembeti ya mulima. 21 Mndewa Mulungu
kamulongela Musa, “Humuluka hasi ukawazume
wanhu wose sekeweze kunilola, buleivo
wezadanganika. 22 Hata wakulu wa nhambiko
wonikwenhukila, wolondeka waisafye, buleivo
niye Mndewa Mulungu nizawatagusa.” 23 Musa
kamulongela Mndewa Mulungu, “Wanhu
hawadaha kukwela mulima wa Sinai kwaviya
kuchizuma weye mwenyewo chike mhaka

kuzunguluka mulima na kuutenda wele.”
24 Mndewa Mulungu kamwidika, “Humuluka
hasi ukamsole Haluni wize nayo. Mbali wakulu
wa nhambiko na wanhu wamwenga sekewaloke
imhaka na kwiza kumwangu, buleivo nizawata-
gusa.” 25 Ivo Musa kahumuluka kwa wanhu na
kawalongela mbuli ziyalagilizigwe na Mndewa
Mulungu.

# 20

### *Ndagilizi longo*

1 Mulungu kalonga mbuli zino zose, kalonga,
2 “Niye Mndewa Mulungu, Mulungu wako
yonikulavile kuna iisi ya Misili, koukalile
mtumwa.
3 “Sekeutambikile milungu imwenga ila niye.
4 “Sekeuitendele nyang'hiti ya chinhu chochose
chilingile fana chinhu cha kuulanga hebu
chili muna iisi hebu chili muna yamazi.
5 Sekeuitumbalile mavindi hebu kuisang'hanila,
kwaviya niye Mndewa Mulungu, Mulungu wako,
ni Mulungu nili na migongo. Nowatagusa wana
kwa uhasanyi wa tati zawo, kwa nyelesi yetatu
na yekane ya waja wonihila. 6 Mbali nolagusa
ulondo wa kufunya umoyo kwa nyelesi maelufu
kwa waja wonilonda niye na kutegeleza ndagilizi
zangu.
7 “Sekeudisang'hanile chakachaka zina da
Mndewa Mulungu, Mulungu wako, mana
Mndewa Mulungu kezamtagusa chila munhu
yodisang'hanila chakachaka zina jake.
8 “Izindilile Siku ya Mhumulo kwa kuitenda
yele, mana ni siku ya chiidumwe. 9 Siku sita

sang'hana usang'hano na utende mbuli zako
zose. 10 Mbali siku yesaba ni Siku ya Mhu-
mulo ya Mndewa Mulungu, Mulungu wako. Siku iyo sekeusang'hane usang'hano wowose, weye hebu mwanago wa chilume hebu mwanago wa chike, hebu wasang'hani wako wa chike hebu wasang'hani wako wa chilume, mnyama wako wa kufugigwa hebu nyambenyambe yeli muna
ikaye yako. 11 Mana kwa siku sita, niye Mndewa
Mulungu nilumba ulanga na isi yose na bahali na vinhu vose vili umo, maabaho siku yesaba nihumula. Ivo niye Mndewa Mulungu niitemela mate siku yesaba na niitenda yele.

12 “Wategeleze tati yako na mami yako, muladi ukale siku nyingi muna iisi ija inikwing'ha niye Mndewa Mulungu, Mulungu wako.

13 “Sekeukome giladi.

14 “Sekeuibandame na mulume hebu muke wa munhu imwenga.

15 “Sekeubawe.

16 “Sekeumulongeleze mkaya miyago kwa mbuli za uvwizi.

17 “Sekeuimelele mate kaye ya munhu imwenga, sekeumelele mate muke wa miyago hebu msang'hani wake wa chike hebu msang'hani wake wa chilume hebu ng'ombe wake hebu chihongwe wake, hebu chinhu chochose chiyeli nacho miyago.”

18 “Wanhu viwahulike mibumo na dizi da mha-
lati na kuwona ng'huwa na yosi kuna mulima,
wagudemeka kwa kudumba na wema kutali.”
19 Wamulongela Musa, “Longa na cheye weye

mwenyewo, chizakutegeleza. Mbali Mulungu sekeyalonge na cheye, buleivo chizadanganika.”

20 Musa kawalongela, “Sekemudumbe, Mulungu keza kumgezani muladi kumtendani mumdumbe na sekemutende uhasanyi.”

21 Lusita Musa viyawile habehi na wingu diya dizamile moyakalile Mulungu, wanhu wose wema kutali.

### *Malagilizo kusonhela lupango*

22 Maabaho Mndewa Mulungu kamulongela
Musa yawalongele Waisilaili, “Muwona mweye
wenyewo kuwa nilonga na mweye kulawa
kuulanga. 23 Sekemuitendele vinhu va hela
vilingile fana Mulungu viwe hamwe na niye,
sekemuitendele milungu ya zahabu hebu shaba.
24 Munhendele lupango lwa ulongo na mulave
nhambiko zenu za wanyama, fana viya nhambiko
ya tindiwalo na nhambiko ya kutimbula.
Chila hanhu hondaniwakumbuse wanhu zina
jangu, nizamwizilani na kumtemelani mate.
25 One mwahazenga lupango lwa mabwe,
sekemuzengele mabwe yosongoligwe, kwaviya
lusita londamusang'hanile mabwe yasongoke,
uhasang'hanila chia chako kusongolela,
kwizakuwa kwambula mwiko. 26 Wala
sekemutende lupango uli na vidando va
kukwelela, muladi munhu yokwela uchanyha
yake sekeyakale mwazi.”

# 21

### *Malagilizo kusonhela watumwa*

1 “Weng'he Waisilaili ndagilizi zino,
2 One uhamgula mtumwa wa Chiebulaniya,
kezakusang'hanila kwa miyaka sita. Mbali
mwaka wa saba kezakuwa kailegeha na kusegela
bila kuliha chochose. 3 One kaguligwa yahawa
hanasola muke, kezasegela yaidumwe. Mbali one
keza na muke wake, basi kezasegela na muke
wake. 4 Mwenevale wake yahamwing'ha muke
na imuke yahamwelekela mwana wa chilume
hebu wa chike, basi imuke na iwana wezakuwa
wa mwenevale, msang'hani iyo kezasegela
yaidumwe. 5 Mbali mtumwa yahalonga,
‘Nomulonda mwenevale wangu na muke wangu
na wanangu, silonda kuilegeha.’ 6 Maabaho
mwenevale wake kezamgala mtumwa iyo
haulongozi wa Mulungu. Kezamsola na kumgala
hana ulwivi hebu chizingiti na kumtobola digutwi
kwa sanziya. Maabaho kezamsang'hanila
mwenevale wake siku zose.

7 “One munhu yahamchuuza mwanage wa
chike kuwa mtumwa, iyo hezatendigwa yailegehe
fana viili kwa mtumwa wa chilume. 8 One ihawa
mwenevale wake kamgula yawe imwe wa wa-
tumwa wake wa chike mbali hanogelwe nayo,
basi mwenevale kezamuleka munhu imwenga
yoyose yamkombole. Mwenevale iyo kabule
haki ya kumchuuza kuna izisi zimwenga, kwa
viya kabena lagano na mtumwa ija. 9 One ya-
halonda kumzengeza mtumwa ija kwa mwan-
age wa chilume, kezamtendela mtumwa iyo fana
mndele wake. 10 One yahasola muke imwenga,
kolondeka yagendelele kumwing'ha muke wake
wa mwanduso ndiya imfaya na viwalo na kwi-

ibandama nayo. 11 One yahapotwa kumtendela
vinhu vino vitatu, muke kosegela kwa kuilegeha
bila kuliha chochose.

### *Malagilizo kusonhela usede*

12 “Munhu yoyose yomtowa miyage na
kumkoma, kolondeka yakomigwe. 13 Mbali
one hamulungile kumkoma ila Mulungu kaleka
ilawilile ivo, basi mkomaji iyo kodaha kukimbilila
hanhu hondaniwasagulileni. 14 Mbali munhu
yahamkoma miyage giladi, hata fana kakimbilila
hana ulupango lwa kuigombela, msegezeni na
mumkome.

15 “Munhu yoyose yomtowa tati yake hebu
mami yake kolondeka yakomigwe.

16 “Munhu yoyose yombawa miyage muladi
yakamchuuze hebu kumtenda yawe mtumwa
wake, kolondeka yakomigwe.

17 “Munhu yoyose yomduwila tati yake hebu
mami yake kolondeka yakomigwe.

18 “Wanhu waidi wahagomba, maabaho
imwenga kamtowa miyage na dibwe hebu
ng'honde bila kumkoma, mbali kamulumiza na
kumtenda yaugule na kutambalala mdikomwa,
19 yahawa munhu iyo yatowigwe kezapata
muhavu na kudaha kugendela mhome, iyo
yamulumize kezalekelelwa. Mbali kezamuliha
kwa lusita loyagize viyakalile mdikomwa na
kolondeka yamuuguze mbaka yahone.

20 “Munhu yahamtowa na balati mtumwa wake
wa chilume hebu wa chike na kumkoma baho
baho, kolondeka yatagusigwe. 21 Mbali mtumwa
iyo yahasigala mgima siku dimwe hebu mbili,

mwenevale wake hezatagusigwa kwaviya kagiza
hela yake iyamgulile.

22 “One walume wahaitowa na kumulumiza
mwanamke yeli na wimo, mbaka kavumbula
siku siyo zake, munhu ija yamulumize kezaliha
fana vondayalonde mulume wa mwanamke iyo
na fana wasemi vondawalamule. 23 Mbali one
kwizalawililа dihile, kezatagusigwa ugima kwa
ugima, 24 ziso kwa ziso, zino kwa zino, mkono
kwa mkono, mgulu kwa mgulu, 25 kulungula kwa
kulungula, chilonda kwa chilonda, kutowa kwa
kutowa.

26 “One munhu yahamtowa muna diziso
mtumwa wake wa chike hebu wa chilume na
kudilava, kolondeka yamuleke yasegele kwa
kuilegeha kwa ichimu cha ziso jake. 27 One
yohamtowa na kumng'ola dizino mtumwa wake
wa chilume hebu wa chike, kolondeka yamuleke
yasegele kwa kuilegeha kwa ichimu cha zino jake.

28 “One ng'ombe yahamkenha mulume hebu
muke na kumkoma, ng'ombe iyo kezakomigwa
kwa kutowigwa na mabwe na nyama yake
haizadigwa. Mwene ng'ombe iyo kezakuwa
kabule mbuli. 29 Mbali one ng'ombe iyo
kazowela kukenha mulume hebu muke na
mwene ng'ombe kalongeligwa mbali hamfungile,
ng'ombe iyo yahakoma mulume hebu muke
kolondeka yatowigwe na mabwe, na mwene
ng'ombe kolondeka yakomigwe. 30 Mbali
munhu iyo yahalongigwa yalave yombe muladi
kuulekelela ugima wake, kolondeka yalihe
chima chiya chondayalongiligwe kulava. 31 One
ng'ombe yahamkenha mbwanga hebu mndele,

izahumizigwa ivo ivo. 32 One ng'ombe iyo
yahamkenha mtumwa wa chilume hebu wa
chike, mwene ng'ombe kezamuliha mwenevale
wa mtumwa iyo kwa shekeli* malongo matatu ya
hela, na ng'ombe iyo kolondeka yakomigwe kwa
kutowigwa na mabwe.
33 “One munhu hadisilize kombo hebu ya-
hahimba kombo na sekeyadigubike, maabaho
ng'ombe hebu chihongwe kodumbukila umo,
34 mwene dikombo ijo kolondeka yamulihe hela
mwene mnyama iyo, na mnyama iyo yafile keza-
kuwa wa mwene dikombo. 35 One ng'ombe
wa munhu yahamulumiza ng'ombe wa munhu
imwenga na kumkoma, wene ng'ombe wezam-
chuuza ng'ombe iyo imgima na kuigolela zi-
hela, iviya wezaigolela ng'ombe yafile. 36 Mbali
one ng'ombe kazowela kuwakenha wayage na
mwene ng'ombe hamfungile, mwenyewo keza-
muliha miyage ng'ombe mgima, ng'ombe yafile
kezakuwa wake.

# 22

*Malagilizo kusonhela maliho*
1 “Munhu yahabawa ng'ombe hebu ng'hondolo
na kumchinja hebu kumchuuza, kolondeka
yalihe ng'ombe watano kwa ng'ombe imwe na
ng'hondolo wane kwa ng'hondolo imwe. 2 Mbavi
yahafikigwa kobena kaye ichilo, yahatowigwa
mbaka kudanganika, yamkomile kabule
ubananzi. 3 Mbali mbavi iyo yahagwiligwa
uchile na kukomigwa, yamkomile kana ubananzi.

* **21:32** Shekeli imwe sawa na gilamu longo na imwe na nusu.

Mbavi iyo kolondeka yabweleze chinhu, one
kabule kolondeka yachuuzigwe muladi kuliha
ubavi wake. 4 One mnyama yabawigwe
yahapatika yahawa mgima kwa mbavi iyo,
basi mbavi iyo kezamuliha miyanza midi, yawe
ng'ombe hebu chihongwe hebu ng'hondolo.

5 “Munhu yahawadima wanyama wake muna
umgunda wa mizabibu na kumulekelela mnyama
wake yaje muna umgunda wa munhu imwenga,
kezaliha udanganyi uwo kwa ndiya inogile ya
umgunda wake mwenyewo hebu mgunda wake
wa mizabibu.
6 “One munhu yahakwacha moto, nawo
uhasoma mibiki ya miwa na kwenela mbaka
kusoma maguniya ya ndiya hebu ndiya za munhu
imwenga zili hazinagoboligwa hebu mgunda
wose wahaka, munhu ija yakwachile moto uwo
kolondeka kuliha udanganyi uwo wose.

7 “One munhu yahamwing'ha miyage chinhu
hebu hela yamwikile goya, maabaho ibawigwa
ukaye yake, mbavi yahapatika kolondeka yal-
ihe hela iyo miyanza midi. 8 Mbali mbavi
one hapatike, mwene kaye kezahita haulon-
gozi ha Mulungu muladi kulonga ukweli kuwa
yeye kamwabule muubavi wa vinhu va miyage.
9 Kwahawa na kuiswela kwa ichimu cha ng'ombe
hebu chihongwe, hebu chinhu chochose chag-
ile, wanhu waidi wolonga ni chawo, wanhu wa-
tendile ivo wezagaligwa haulongozi wa Mulungu.
Munhu ija Mulungu yondayalamule kuwa ka-
bananga, kezamuliha miyage miyanza midi.

10 “Munhu yahamwing'ha miyage ng'ombe
hebu ng'hondolo hebu chihongwe hebu mnyama

imwenga yoyose yamulole goya na mnyama
iyo yahafa hebu yahalumila hebu yahasoligwa
bila munhu imwenga kumuwona, 11 chilaho
haulongozi wa Mndewa Mulungu chizalamula
hagati yawo kulagusa kuwa iyo yeng'higwe
kamwabule muubavi wa vinhu va miyage.
Mwene mnyama iyo kezatogola chilaho icho,
na iyo miyage hezaliha chochose. 12 Mbali
one ihamanyika kuwa mnyama kabawigwa
kumwake, imunhu iyo kolondeka yamulihe
mwene mnyama. 13 One kakomigwa na
wanyama wa kumbago, munhu iyo kolondeka
yamgale imnyama fana usindila, halondeka
kuliha chochose kwa mnyama yoyakomigwe
na wanyama wa kumbago.

14 “One munhu yahazima mnyama kwa miyage,
maabaho mnyama iyo kalumila hebu kafa, lusita
mwene mnyama kahabule, ija yazime kolondeka
yamulihe mnyama fana ija. 15 Mbali one ilawilila
mwene mnyama kabaho, yazime hezaliha cho-
chose. One kakala yazimigwe kwa hela, hela izo
zizafaya kwa kwaga kwa mnyama iyo.

## *Malagilizo ya kukala na wanhu*

16 “Munhu yahamvwizila mhambe yeli
hanauzigwa na kambandama, kolondeka
yamfungile zengele na kumsola yawe muke
wake. 17 Tata wa mndele iyo yahalema ng'hani
kumzengeza mwanage, munhu iyo kezaliha hela
ya zengele yoilondeka kwa mndele yeli mhambe.

18 “Sekeumuleke mwanamke muhawi yawe
mgima.

19 “Munhu yoyose yoibandama na mnyama kolondeka yakomigwe.

20 “Munhu yoyose yomulavila nhambiko mulungu imwenga badala ya Mndewa Mulungu muhala, kolondeka yakomigwe.

21 “Sekeumbamanye nyambenyambe
hebu kumgaza, mana na mweye iviya
mukala nyambenyambe muna iisi ya Misili.
22 Sekeumgaze mgane yoyose hebu mwana
mchiwa. 23 One uhawabamanya nawo
wahanyulululuka, ukweli nizahulika ndilo yawo.
24 Nizakuwa na ludoko ng'hani na nizamkomani
na panga. Wake zenu wezakuwa wagane na
wanenu wezakuwa wachiwa.

25 “Uhamwazima hela munhu yoyose mwa
iwanhu wangu weli ngayengaye, sekeuwe fana
mdai, iviya sekeulonde yakulihe limangwe.
26 One uhasola mgolole wa miyago na kuwika
poni, kolondeka umbwelezele ding'hali zuwa
hadinahonga. 27 Kwaviya mgolole wake wa
kuigubika uwo muhala. Vino weye kogesa
kezaigubika choni? Yahanililila nizamwidika
kwaviya niye nina ubazi.

28 “Sekeumulige Mulungu hebu sekeumduwile mtawala wa wanhu wako.

29 “Sekeukalame kulava nhosa mvunyo kulawa
muna yamalimbulo ya mavuno yako na mal-
imbulo ya divai yako. Mwizaning'ha wanenu
waudele wa chilume. 30 Mwizatenda ivo ivo kwa
waudele wa ng'ombe na ng'hondolo wenu. Chila
mwelekwa wa udele mwizamuleka na mami yake
kwa siku saba, siku yenane mwizaning'ha niye.

31 “Mweye mwizakuwa wanhu wangu
waidumwe. Ivo sekemuje nyama ya mnyama
yakomigwe na mnyama wa kumbago. Nyama iyo
mwizawasila zimbwa.

# 23

*Kuleka kubagula*

1 “Sekeupwililise mbuli za uvwizi, na sekeum-
taze munhu mbananzi kwa kulava ukalangama
wa uvwizi. 2 Sekeusondelele bumbila da wanhu
kutenda mbuli zihile, hebu sekewiilumbe na
wanhu kulava ukalangama muna ichitala muladi
kwagiza ukweli. 3 Sekeuwonele muna imbuli ya
ngayengaye.

4 “Uhamfika ng'ombe hebu chihongwe wa
mwihi wako kaga, mbwelezele mwenyewo. 5 One
uhamuwona chihongwe wa munhu yokwihila
kagwa na mbahasha yake, sekeumuleke mtaze.

6 “Sekeuyagize haki iyolondeka kupata
ngayengaye muna imbuli yake. 7 Iteganye
sekeumulongeleze munhu uvwizi na
sekeumkome munhu yelibule ubananzi, kwa
viya Mulungu hezawalekelela wanhu wabananzi.
8 Sekeuhokele chinhu cha kukutenda ubene
malagilizo, kwaviya chinhu icho chowatula
yameso wanhu weli na ubala na kuwagiza wanhu
wanogile.

9 “Sekeumbamanye nyambenyambe, mweye
muumanya unyambenyambe, mana na mweye
mukala nyambenyambe muna iisi ya Misili.

*Malagilizo ya kusonhela Siku ya Mhumulo na dugila*

10 “Kwa miyaka sita kwizahanda migunda yako
na kwaha vinhu vihandigwe. 11 Mbali muna
umwaka wa saba, kwizaleka migunda yako yose bila ya kuhanda mbeyu muladi ngayengaye weli mwa wanhu wako wapate ndiya isigale umo na wanyama wa kumbago waje. Kwizatenda ivo ivo muna umgunda wako wa mizabibu na mizaituni.

12 “Kwa siku sita kwizasang'hana sang'hano zako, mbali siku yesaba uhumule, muladi ng'ombe wako na vihongwe wako iviya wahumule, na watumwa wowelekigwe muna ikaye yako na nyambenyambe wahumule.

13 “Tegeleza chila chinhu chonikulongela. Sekeuyatambule mazina ya milungu imwenga hata chidogo, mazina yayo sekeyahulikike muna umulomo wako.

*Madugila matatu makulu*

14 “Miyanza mitatu chila mwaka mwizatenda
madugila kwa hishima yangu. 15 Mwizagendelela
kutenda Dugila da Magate Hayagumigwe Lusu fana vinimulagilizeni, mwizakuja magate hayagumigwe lusu kwa siku saba lusita lwikigwe muna umwezi wa Abibu, kwaviya muna umwezi uwo mulawa Misili. Munhu yoyose sekeyeze haulongozi wangu makono muhala.
16 Mwizagendelela kutenda Dugila da Vinhu va Mwanduso vimugobole muna imigunda yenu. Mwizatenda Dugila da Kuduganya Vinhu Vimugobole kuuhelelo wa mwaka vondamuduganye vinhu venu vimuhandile.
17 Miyanza mitatu kwa mwaka walume wose

wezalawilila haulongozi wa Mndewa Mulungu, Mndewa yeli na udahi.
18 “Sekeulave damu ya nhambiko yangu hamwe na magate yagumigwe lusu, na sekeuyaleke mavuta ya mnyama ya dugila jangu yasigale mbaka imitondo.
19 “Ndiya ya mwanduso ya isi yako kwizaigala kuna ikaye ya Mndewa Mulungu, Mulungu wako.
“Sekeumkimuse mwanaluti muna yamatombo ya mami yake.

### *Msenga wa Mulungu kosasala nzila*

20 “Lola, nomtuma msenga wa kuulanga kuulongozi wenu muladi yamkalizeni mzila na
kumgalani kuna iisi yoniisasale. 21 Mtegelezeni
na kwamha choyolonga sekemumwehule, hezawalekelelani ubananzi wenu, kwaviya nahamwe
nayo. 22 Mbali muhamtegeleza chiyolonga na
kutenda yose yonimulongelani, nizakuwa mwihi wa wehi wenu na nizawalema wose womulemani mweye.
23 “Msenga kuulanga kezamulongolelani na kumgalani kuna iisi ya Waamoli na Wahiti na Wapelizi na Wakanaani na Wahivi na Wayebusi,
nawo nizawadanganiza. 24 Sekemutumbale
mavindi kuitambikila milungu yawo hebu kuisang'hanila hebu sekemuhige sang'hano zawo. Mwizawadanganiza na kuvibomola
vibanda vawo. 25 Nisang'hanileni niye Mndewa
Mulungu, Mulungu wenu, niye nizamtemelani mate kwa ndiya na mazi na kusegeza mitamu
kumwenu. 26 Hakwizakuwa na mwanamke
yondayatengule hebu kuwa mgumba muna iisi yenu. Nizamtendani mukale siku nyingi ng'hani.

27 “Nizawadumbiza na kuwatibula wanhu
wose womuitowa nawo, wehi wenu nizawatenda
wahinduke na kukimbila. 28 Nizawawinga
Wahivi na Wakanaani na Wahiti fana wanhu
viwowingigwa na madondola. 29 Wanhu
wawo sizawawinga muna umwaka umwe,
kwaviya isi izasigala yabule chinhu na
wanyama wa kumbago wezakongezeka ng'hani.
30 Mbali nizawasegeza chidogo chidogo mbaka
vondamongezeke na kuitawala isi yose.

31 “Mhaka za isi yenu zizakuwa kulawa bahali
ya Shamu mbaka bahali ya Meditelaniya,
na kulawa kuchuwala mbaka lwanda lwa
Efulati, mana wakaya wa isi iyo nizawatenda
muwahume, na mweye mwizawawinga wasegele
kumwenu. 32 Sekemutende nawo lagano jojose
hebu na milungu yawo. 33 Sekemuwaleke
wakale muna iisi yenu, buleivo wezamtendani
munihasanye, mana muhaitambikila milungu
yawo, kweli kumwenu uwo wizakuwa mtego wa
kunamata.”

# 24

## *Lagano dolagusigwa*

1 Maabaho Mndewa Mulungu kamulongela
Musa, “Kweleni kumwangu, weye na Haluni
na Nadabu na Abihu, hamwe na walala
malongo saba wa Isilaili, munitumbalile mavindi
kwa kutali. 2 Mbali weye Musa wiidumwe
ukwenhuke habehi na Mndewa Mulungu,
wayago sekewakwenhuke habehi. Wanhu
sekeweze hamwe na weye.”

3 Musa kahita na kuwalongela wanhu mbuli
zose za Mndewa Mulungu na ndagilizi zose,
wanhu wose wedika kwa dizi dimwe, walonga,
“Chizatenda chila chinhu chiyalongile Mndewa
Mulungu.” 4 Musa kandika chila chinhu chiya-
longile Mndewa Mulungu. Igolo yake kaidawa na
kazenga ulupango hasi ya mulima na kasimika
mhanda longo na mbili fana viili peta ya maka-
bila longo na maidi ya Isilaili. 5 Maabaho kawa-
tuma wabwanga wa Waisilaili wamulavile Mn-
dewa Mulungu nhambiko za kutimbula na nham-
biko za tindiwalo za ng'ombe lume. 6 Musa ka-
sola nusu ya damu ija na kaiguma muna yama-
hamha, nusu imwenga kaitila uchanyha ya ulu-
pango. 7 Maabaho kasola chitabu cha lagano
na kawasomela wanhu. Nawo wedika, “Chiza-
tenda chila chinhu chiyalongile Mndewa Mu-
lungu, chizazindililа.” 8 Musa kasola damu ija
na kawamizila wanhu, kalonga, “Ino iyo damu
ya lagano da Mndewa Mulungu diyatendile na
mweye kwa kuisondelela na mbuli zino zose.”
9 Musa na Haluni na Nadabu na Abihu, hamwe
na walala malongo saba wa Waisilaili wakwela
kuumulima 10 na wamuwona Mulungu wa Isilaili.
Hasi ya migulu yake hakala na chinhu chilingile
fana sakafu ya mabwe ya yakuti ya langi ya bu-
luu fana ulanga. 11 Mbali Mulungu hawalumize
walangulizi wawo wa Isilaili. Wamuwona Mu-
lungu na waja na kung'wa.

### *Musa kuna mulima wa Sinai*

12 Mndewa Mulungu kamulongela Musa, “Izo
kumwangu kuchanyha ya mulima ukale kuno,

nizakwing'ha vibawo vidi va mabwe vili na
malagilizo na ndagilizi zonyandike kwa ichimu
cha kuwafunza Waisilaili."
13 Ivo Musa kasegela hamwe na Yoshua
msang'hani wake, na Musa kakwela kumulima
wa Mulungu. 14 Musa kawalongela walala,
"Chigozeleni hano mbaka vondachibwele. Haluni
na Huli wezakuwa bahano na mweye, yoyose
yondayawe na mbuli kodaha kuwahitila wawo."
15 Musa kakwela kuna mulima, maabaho wingu
digubika mulima. 16 Utunhizo wa Mndewa Mu-
lungu uhumuluka kuna mulima wa Sinai. Wingu
diugubika mulima kwa siku sita. Siku yesaba
Mndewa Mulungu kamtanga Musa kulawa hagati
ya diwingu. 17 Kuwoneka kwa utunhizo uja wa
Mndewa Mulungu kuwa fana moto woulunguza
hachanyha ya mulima muna yameso ya wanhu
wa Isilaili. 18 Musa kengila muna diwingu na kak-
wela kumulima. Kakala kumulima siku malongo
mane imisi na ichilo.

# 25

## *Nhambiko kwa ichimu cha hema da Mulungu*

1 Mndewa Mulungu kamulongela Musa,
2 "Walongele Waisilaili wanilavile nhosa.
Nihokelele nhosa zangu kulawa kwa munhu
yoyose yolonda kuning'ha. 3 Zino niizo nhosa
zondauzihokele kulawa kumwawo, zahabu na
hela na shaba 4 na langi ya buluu na langi ya
zambalau na langi ndung'hu na viwalo vinogile
na mazoya ya luti 5 na mbende za mabebelu
ya ng'hondolo zihakigwe langi ndung'hu, na
mbende za wanyama wa mwiibahali na mibiki

ya mkenge, 6 na mavuta ya chitasa cha hema da
Mulungu, vilungo kwa mavuta yelile na ubani,
7 na mabwe yokwaka ya salidoniki na mabwe
yokwaka yamwenga kwa ichimu cha mahambo,
chifuko cha muimhambaga na chizibawo cha
mkulu wa nhambiko. 8 Leka wanhu wanizengele
hanhu helile, muladi nidahe kukala hamwe
nawo. 9 Zenga hema da Mulungu na vinhu vake
vose kuilinga na viya vondanikulaguse.

### *Sanduku da lagano*

10 “Nawo watende sanduku da mbiki wa
mkenge, utali wake uwe sentimita gana na longo,
ugalamu wake sentimita malongo sita na sita
na chimo chake iwe sentimita malongo sita na
sita. 11 Na weye udihake zahabu yelile mgati
na kunze, uditendele lukingilo lwa zahabu banzi
zose. 12 Maabaho utende mhete nne za zahabu
na uzivaze muna imigulu yake mine, mhete mbili
banzi imwe na banzi imwenga mhete mbili. 13 Na
utende mibiki ya kupapila ya mkenge na uihake
zahabu. 14 Ingiza mibiki iyo muna zimhete zili
banzi mbili za sanduku, kwa ichimu cha kudi-
papa. 15 Mibiki iyo ya kupapila izasigala muna
zimhete, sekeisegezigwe. 16 Muna disanduku ijo,
kwizakwika vibawo va mabwe va ukalangama
vondanikwing'he.

17 “Tenda ngubiko ya zahabu hanhu ha
kuilumba, utali wake wizakuwa sentimita
gana na longo na ugalamu wake sentimita
malongo sita na sita. 18 Tenda vilumbe vidi va
zahabu vovilingile fana wasenga wa kuulanga,
tenda usang'hano wa kuhonda muna imihelelo
ya ingubiko iyo. 19 Tenda vilumbe ivo vidi,

chimwe uhelelo umwe na chimwenga uhelelo
wekaidi, tenda vilumbe ivo vidi chinhu chimwe
na ngubiko. 20 Vilumbe wawo wezailola,
mabawa yawo yakunjuka kuigubika ingubiko,
vihanga vawo vizailola ingubiko iyo. 21 Mgati
mudisanduku kwizakwika vibawo vidi va mabwe
va ukalangama na kuika ngubiko iyo uchanyha
yake. 22 Nizaiting'hana na weye baho, kulawa
hachanyha ya ngubiko iyo, hagati ya vilumbe
wawo waidi weli mchanyha ya sanduku da
lagano, nizakwing'ha malagilizo yangu kwa
ichimu cha wanhu wa Isilaili.

### *Meza kwa ichimu cha magate ya nhosa ya Mndewa Mulungu*

23 “Songola meza ya mibiki ya mkenge, yili
na utali wa sentimita malongo manane na nane
na ugalamu sentimita malongo mane na nne
chimo sentimita malongo sita na sita. 24 Meza
iyo kwizaihaka zahabu yelile na kuizungulusila
lukingilo lwa zahabu. 25 Maabaho kwizaizun-
gulusila lukingilo lwili na ugalamu wa sentimita
nane. 26 Kwizaitendela mhete nne za zahabu na
kuzika kuna zimhembe zake muna imigulu yake.
27 Mhete izo zizakuwa habehi na lukingilo luja lwa
kuzunguluka meza na zizakuwa za kwamhilila
mibiki ya kupapila imeza iyo. 28 Tenda mibiki ya
kupapila ya mkenge na kuihaka zahabu, mibiki
iyo izakuwa ya kuipapila meza iyo. 29 Tengeneza
vyano na nhungo na mabuyu na vihamha va
kugidila. Tengeneza via ivo vose kwa zahabu
yelile. 30 Chila siku ika magate yelile hana imeza
haulongozi hangu.

*Chinala cha chitasa*

31 “Kwizatenda chinala cha chitasa kwa zahabu
yelile. Itendigwe kwa kuhonda, kalilo jake na
mbiki wake na nhungo zake na matumba yake
na maluwa yake, vose vizatendigwa kwa chi-
hande chimwe. 32 Matambi sita yezalawilila hana
umbiki wa ichinala, matambi matatu ubanzi
umwe na matambi matatu ubanzi umwenga.
33 Muna ditambi kuna nhungo nhatu zilingile
fana matumba na maluwa yotangigwa alimondi,
muna ditambi disondelela kuna tumba jake na
luwa jake. Matambi yose sita yawe fana ivo.
34 Na muna ichinala kwizakuwa na nhungo nne
zozitendigwe zilingile fana maluwa yotangigwa
alimondi, hamwe na ving'honyo va maluwa yake.
35 Hanhu hondahalawilile chila jozi ya matambi
yaja sita, hasi yake hezakuwa na tumba dimwe
dimwe. 36 Matumba yayo na matambi yake yeza-
kuwa chinhu chimwe. Chinala icho chose chiza-
hondigwa kwa zahabu yelile. 37 Iviya kwiza-
tenda vitasa saba kwa ichimu cha chinala icho
na kuvika uchanyha yake muladi vimwemwese
kuulongozi. 38 Tengeneza makoleo yake na vyano
vake kwa zahabu yelile. 39 Sang'hanila chilo ma-
longo matatu na tano va zahabu yelile kuten-
geneza chinala cha chitasa na via vake vose.
40 Hakikisha uvitengeneze fana viya vinikulaguse
kuja kumulima.

# 26

*Hema jelile*
*(Kulawa 36:8-38)*

1 “Maabaho zenga hema da Mulungu kwa
mapanzia longo ya mawalo yanogile yabotigwe
kwa nyuzi za langi ya buluu na za zambalau na
ndung'hu. Mapanzia yayo kwizayahamba kwa
vilumbe walingile fana wasenga wa kuulanga wa-
songoligwe na fundi. 2 Chila panzia dizakuwa na
utali wa mita longo na mbili na ugalamu mita
mbili. 3 Kwizalumbiliza mapanzia matano yawe
chihande chimwe, mapanzia yamwenga matano
yawe chihande chekaidi. 4 Iviya kwizasonela vi-
tanzi va buluu muimhindo ya dipanzia da uhelelo
da chihande cha mwanduso, iviya kwizashona
vitanzi kuuhelelo wa mhindo ya kunze ya chi-
hande chimwenga cha panzia. 5 Kwizagela vitanzi
malongo matano muna dipanzia dimwe, vitanzi
vimwenga malongo matano va panzia dekaidi,
vitanzi vose viilole. 6 Maabaho kwizatengeneza
vihindo malongo matano va zahabu muladi ku-
lumbiliza viya vihande vidi va mapanzia, ivo
hema da Mulungu dizakuwa chinhu chimwe.

7 “Iviya kwizatengeneza ngubiko imwenga ya
hema da Mulungu kwa mapanzia longo na dimwe
ya mazoya ya luti. 8 Chila panzia dizakuwa na
utali wa mita longo na nhatu na ugalamu wake
mita mbili, mapanzia yose longo na imwe yeza-
kuwa na ningo ziya ziya. 9 Kwizalumbiliza ma-
panzia matano hamwe na mapanzia sita hamwe,
panzia desita kwizadibanda haulongozi wa hema
ijo. 10 Maabaho kwizatenda vitanzi malongo
matano muimhindo ya panzia da uhelelo da chi-
hande cha mwanduso, kwizatenda vitanzi mal-
ongo matano muimhindo ya panzia ya uhelelo wa
chihande chekaidi. 11 Kwizatengeneza vihindo

malongo matano va shaba na kuzigela muna iv-
itanzi viya malongo matano muladi kulumbiliza
vihande vidi va mapanzia kutenda panzia dimwe
da hema. 12 Nusu ya panzia disigale, kwizai-
tumbika ubanzi wa kuchisogo wa dihema, 13 Utali
wa panzia disigale kwizaibanda nusu mita ubanzi
umwe na nusu mita ubanzi umwenga, muladi
itinge ubanzi wa dihema muladi iwe na ngubiko.

14 “Kwizatengeneza ngubiko imwenga ya hema
kwa mbende ndung'hu ihondigwe ya mabebelu
ya ng'hondolo na mchanyha yake ngubiko
imwenga ya mbende ya mnyama wa mwiibahali.

15 “Kwizatengeneza mibiki ya mkenge ya
kwimizila dihema. 16 Mibiki izakuwa na utali
wa mita nne na ugalamu wa sentimita malongo
sita na sita, 17 mibiki izakuwa na ndimi mbili za
kulumbilizila. Mibiki yose kwizaitenda iwe na
ndimi mbili. 18 Kwizatengeneza mibiki ya hema
vino, mibiki malongo maidi ubanzi wa kusi 19 na
vikalilo malongo mane va hela hasi ya mibiki iyo
malongo maidi, vikalilo vidi hasi kwa chila mbiki
muladi vamhilile ndimi zake mbili na vikalilo vidi
viwe hasi ya mbiki umwenga muladi wamhilile
ziya ndimi zake mbili. 20 Ubanzi wa kasikazi wa
hema kwizatengeneza mibiki malongo maidi
21 Na vikalilo vake malongo mane va hela,
vikalilo vidi hasi ya chila mbiki. 22 Kwa ubanzi
wa kuchisogo wili uswelo wa zuwa wa hema
kwizatengeneza mibiki sita. 23 Na kwizatenda
mibiki midi kwa ichimu cha vingobweda va
dihema ubanzi wake wa kuchisogo. 24 Mibiki iyo
ya hasi iileke mbali ilumbilizigwe kwa kuchanyha
kuna imhete imwe. Mibiki yose ya vingobweda

izatendigwa ivo ivo muladi itende mbili. 25 Ivo
kwizakuwa na mibiki minane hamwe na vikalilo
vake longo na sita va hela.

26 “Kwizatengeneza mapalo ya mkenge, ma-
palo matano kwa ichimu cha mibiki ya ubanzi
umwe wa hema, 27 mapalo matano kwa ichimu
cha ubanzi umwenga wa hema, mapalo matano
kwa ichimu cha mibiki ya kuchisogo cha hema
na ubanzi wa uswelo wa zuwa. 28 Palo da hagati
dodifikile nusu ya zengo da hema dizaibebenyeka
hagati kulawa kuuhelelo umwe mbaka uhelelo
umwenga wa hema. 29 Mibiki yose kwizaihaka
zahabu na kuzitendela mhete za zahabu zon-
dazamhilile mapalo yayo, izo iviya kwizazihaka
zahabu. 30 Ivo kwizaditenda hema ijo kuilinga na
viya vinikulaguse kumulima.

31 “Kwizatenda panzia da nyuzi za langi ya
buluu na za zambalau na ndung'hu na walo di-
botigwe. Panzia ijo kwizadihamba vinogile kwa
vilumbe vilingile fana wasenga wa kuulanga wa-
songoligwe na mafundi. 32 Kwizatumbika di-
panzia muna izimhanda nne za mkenge zozi-
hakigwe zahabu, zili na ngwamo za zahabu na
vikalilo vine va hela. 33 Kwizatumbika panzia
ijo muna ivihindo, maabaho udigale disanduku
diya da ukalangama dili na vibao vidi va mabwe
kuchisogo ya panzia ijo. Panzia ijo dizagola
hanhu helile na hanhu helile ng'hani. 34 Ika ngu-
biko uchanyha ya disanduku da lagano mgati ya
hanhu helile ng'hani. 35 Meza ija kwizaika ubanzi
wa kunze wa panzia ijo, chinala chiya cha chitasa
kwizachika ubanzi wa kusi wa dihema, viilole na
imeza. Meza iyo izakuwa ubanzi wa kasikazi.

36 “Kwa ichimu cha hanhu ha kwingilila muna
dihema kwizatengeneza panzia da langi ya bu-
luu na zambalau na ndung'hu na walo dinogile
dibotigwe na kuhambigwa vinogile. 37 Kwa
ichimu cha panzia kwizatengeneza mhanda tano
za mkenge na kuzihaka zahabu. Mhanda izo ziza-
kuwa na ngwamo za zahabu, chila imwe izakuwa
na kalilo da shaba.”

# 27

### *Upango*
### *(Kulawa 38:1-7)*

1 “Tengeneza upango kwa mibiki ya mkenge.
Ulupango uwo wizakuwa wa mulaba utali wake
mita mbili na lobo na ugalamu wake mita mbili
na lobo na chimo chake chizakuwa mita imwe na
lobo. 2 Kwizatenda mahembe mane, chila chin-
gobweda hembe dimwe. Mahembe yayo yeza-
kuwa chinhu chimwe na ulupango, kwizaluhaka
shaba ulupango lose. 3 Kwizatenda via vake, vizae
va kuzolela maivu na vizae va kuhalila moto na
mibatilo na magembe na vyano va kuhalila moto.
Vinhu vose vizahakigwa shaba. 4 Maabaho kwiz-
atengeneza lwavu lwa shaba lwili na mhete nne
za shaba kuna ivingobweda vake vine. 5 Lwavu
ulo kwizawika mulugigo lwa ulupango ubanzi wa
hasi muladi lwavu lufike hagati ya upango. 6 Na
kwizatengeneza mibiki ya mkenge ya kupapila
ulupango, nayo kwizaihaka shaba. 7 Mibiki iyo
izakwingizigwa muna zimhete banzi mbili za ulu-
pango lusita lwa kuchipapa. 8 Tengeneza upango
wa mibiki na uli na uvungu mgati kuilinga na
simwe donikulaguse kumulima.

### *Luwa lwa hema da Mulungu*

9 “Tengeneza luwa lwa hema da Mulungu.
Ubanzi wa kusi wa uluwa kwizakuwa na ma-
panzia yatengenezigwe kwa walo dinogile di-
botigwe yondayawe na utali wa mita malongo
mane na nne kwa ubanzi umwe. 10 Mapanzia
yayo yezakwamhigwa na mibiki malongo maidi
ya shaba ili na vikalilo va shaba. Mbali ngwamo
za mhanda na vihindo vake vizakuwa va hela.
11 Iviya utali wa panzia ubanzi wa kasikazi wiz-
akuwa mita malongo mane na nne na mhanda
zake malongo maidi za shaba, mbali ngwamo
na mhanda zake na vihindo vake vizakuwa va
hela. 12 Ubanzi wa uswelo wa zuwa wa uluwa
wizakuwa na panzia dili na utali wa mita mal-
ongo maidi na mbili na mhanda zake longo na
vikalilo vake longo. 13 Ubanzi wa ulawilo wa
zuwa kuna ulwivi, luwa lwizakuwa na ugalamu
wa mita malongo maidi na mbili. 14 Panzia da
ubanzi umwe wa ulwivi dizakuwa na ugalamu wa
mita sita na nusu, hamwe na mhanda nhatu na
vikalilo vake vitatu. 15 Kuna ubanzi wekaidi wa
lwivi panzia dizakuwa mita sita na nusu, hamwe
na mhanda tatu na vikalilo vake vitatu. 16 Lwivi
lwenyewo lwa uluwa lwizakuwa na panzia dili na
utali wa mita kenda, ditengenezigwe kwa nyuzi
za langi ya buluu na za zambalau na ndung'hu na
walo dinogile dibotigwe na kuhambigwa vinogile.
Panzia ijo dizakwamhigwa na mhanda nne zili na
vikalilo vine. 17 Mhanda zose zizunguluke uluwa
zizakwamhigwa na vinhu va hela, ngwamo zake
zizakuwa za hela na vikalilo vake vizakuwa va
shaba. 18 Luwa ulo lwizakuwa na utali wa mita
malongo mane na nne na ugalamu wa mita ma-

longo maidi na mbili, chimo mita mbili na lobo.
Mapanzia yake yezakuwa ya walo dinogile na
vikalilo vake vizakuwa va shaba. 19 Via vose
va kusang'hanila chila chinhu muna dihema da
Mulungu na vigingi vose na hata via va uluwa
vizakuwa va shaba.

### *Kwika goya chitasa (Walawi 24:1-4)*

20 “Walagilize wanhu wa Isilaili wakugalile
mavuta yanogile ya mzaituni kwa ichimu cha
chitasa, muladi chitasa chidahe kwaka lusita lose.
21 Muna dihema da Mulungu kunze ya panzia
ijo haulongozi ha sanduku da lagano, Haluni na
wanage wezadika goya haulongozi ha Mndewa
Mulungu ichigulogulo mbaka imitondo. Lagilizo
dino dolondeka jamhigwe na Waisilaili wose na
nyelesi zawo siku zose.

# 28

### *Mawalo ya wakulu wa nhambiko (Kulawa 39:1-7)*

1 “Mgale Haluni ndugu yako na wanage,
Nadabu na Abihu na Eleazali na Isamali.
Wagale kulawa mwa wanhu wa Isilaili muladi
wanisang'hanile fana wakulu wa nhambiko.
2 Kwizamsonela Haluni ndugu yako mawalo
yelile muladi yadahe kuwoneka yeli na utunhizo
na kanoga. 3 Walagilize wanhu wose weli na
umanyi woniweng'hile ubala wamsonele Haluni
mawalo, muladi yadahe kubaguligwa kuwa
mkulu wa nhambiko muna usang'hano wangu.
4 Walongele wamtendele mawalo yelile, chifuko
cha muimhambaga na chizibawo na ng'hanzu

na chilemba na mkwiji na joho dodihambigwe.
Haluni ndugu yako na wanage wezavala muladi
wanisang'hanile fana wakulu wa nhambiko.
5 Wezasang'hanila nyuzi za langi ya buluu na za
zambalau na ndung'hu na nyuzi za zahabu na
walo dinogile ibotigwe.

6 “Wezatengeneza chizibawo cha mkulu wa
nhambiko kwa nyuzi za zahabu na nyuzi za
langi ya buluu na za zambalau na ndung'hu na
walo dinogile dibotigwe na fundi. 7 Chizakuwa
na nzabi mbili za kuchifungila muna diyega
zozisonigwe hamwe muna zimhembe zake mbili.
8 Mkwiji wizatendigwa fana viya, kwa nyuzi za
zahabu na nyuzi za buluu na za zambalau na
ndung'hu na walo dinogile dibotigwe na kuwa
chinhu chimwe na chizibawo icho. 9 Maabaho
kwizasola mabwe maidi ya salidoniki na
uchanyha yake kwizachola mazina ya wana wa
Isilaili. 10 Mazina sita muna idibwe da mwanduso
na mazina sita muna idibwe dekaidi, uyapange
fana viya viwelekigwe. 11 Kwizayachola mazina
yayo uchanyha ya mabwe yayo fana viya sonala
viyochola muhuli. Maabaho uyahambe na
kuyengiza muna ivihindo va zahabu. 12 Mabwe
yayo maidi yezakwikigwa uchanyha ya vihande
va muna yamayega va chizibawo kulagusa
makabila longo na maidi ya Isilaili. Ivo Haluni
kezavala mazina yayo muna yamayega yake
haulongozi wangu niye Mndewa Mulungu
fana lukumbuso. 13 Kwizatenda vihindo vidi
va zahabu, 14 na mikufu midi ya zahabu yelile
ibotigwe fana luzabi. Kwizaifunga mikufu iyo
muna ivihindo.

### *Chifuko cha mwiimhambaga (Kulawa 39:8-21)*

15 “Kwizatenda chifuko cha muimhambaga cha
kuhumiza, chitengenezigwe na fundi fana vi-
chitengenezigwe chiya ichizibawo, kwa zahabu
na kwa nyuzi za langi ya buluu na za zambalau na
ndung'hu na walo dinogile dibotigwe. 16 Chifuko
icho chibandigwe chizakuwa cha mulaba, sen-
timita malongo maidi na mbili. 17 Chizahambigwa
kwa misitali mine ya mabwe ya bei ng'hulu. Msi-
tali wa mwanduso wizakuwa wa hakiki na topazi
na alimasi ndung'hu. 18 Msitali wekaidi wiza-
kuwa wa zumalidi na johali ya langi ya buluu
na alimasi ya langi ya mayani mabisi. 19 Msitali
wekatatu wizakuwa wa yasito na agate na ame-
sisito. 20 Msitali wekane wizakuwa wa zabalajadi
na shohamu na yasipi, yose yezagumigwa muna
ivihindo va zahabu. 21 Lelo hezakuwa na mabwe
longo na maidi yoyacholigwe mazina longo na
maidi ya wana wa Isilaili. Chila dimwe dizakuwa
fana uhula muladi kulagusa makabila longo na
maidi.

22 “Kwa ichimu cha chifuko icho cha
muimhambaga, kwizatengeneza mikufu
ya zahabu yelile ibotigwe fana luzabi.
23 Iviya kwizachitengenezela ichifuko cha
muimhambaga mhete mbili za zahabu na
kuziguma muna zimhembe mbili za chifuko
icho. 24 Na uigume imikufu midi ya zahabu
muna zimhete izo za chifuko cha muimhambaga.
25 Zinhonga ziya mbili za mikufu ya zahabu
kwizazigeleka muna ivihindo vidi muladi
ziigelekeze na ichihande cha muna yamayega

cha chizibawo ubanzi wa kuulongozi.
26 Iviya kwizatengeneza mhete mbili za zahabu na kuziguma muna zimhembe mbili za hasi, ubanzi wa mgati wa chifuko cha muimhambaga habehi na ichizibawo.
27 Maabaho kwizatengeneza mhete zimwenga mbili za zahabu na kuziguma kuulongozi muna zimhembe mbili za hasi za vihande va muna yamayega va chizibawo, hanhu chizibawo hochiilumba na mkwiji woubotigwe vinogile.
28 Chifuko cha muimhambaga chizafungigwa kuna ichizibawo kwa kulumbiliza mkwiji wake na chizibawo kwa luzabi lwa langi ya buluu, muladi chifuko icho cha muimhambaga sekechitohoke mbali chikale muna ichizibawo.
29 “Haluni viyokwingila hanhu helile, kezavala chifuko cha muimhambaga cha kuhumiza chicholigwe mazina ya makabila ya wana wa Isilaili, kwa kutenda ivo, niye Mndewa Mulungu sizawazimiza ng'o.
30 Kwizaguma Ulimu na Sumimu muna ichifuko cha muimhambaga cha kuhumiza, izo zizakuwa uchanyha ya moyo wa Haluni chila viyokwiza haulongozi wangu. Haluni kezasola ulamuzi wa wana wa Isilaili wawo uchanyha ya moyo wake haulongozi wa Mndewa Mulungu siku zose.

### *Mawalo yamwenga ya ukulu wa nhambiko (Kulawa 39:22-31)*

31 “Kwizasona joho da kuvalila chizibawo kwa nyuzi za langi ya buluu.
32 Hagati izakuwa na nyafasi ya kufosezela ditwi, nyafasi iyo izasonigwa na nyuzi muladi sekeidegeke.
33 Muna imhindo yake ya hasi kuzunguluka banzi zose, izacholigwa makomamanga ya langi ya buluu na

zambalau na ndung'hu, iviya hagati ya mako-
mamanga yayo hezakuwa na mbugi za zahabu.
34 Komamanga na mbugi ya zahabu kuzunguluka
joho yose. 35 Haluni kolondeka yavale ng'hanzu
ino lusita viyosang'hana usang'hano wa ukulu wa
nhambiko. Dizi da mbugi dizahulikika viyok-
wingila hanhu helile haulongozi ha Mndewa Mu-
lungu na viyolawa, ivo hezakomigwa bule.

36 “Maabaho kwizatengeneza chihande cha za-
habu yelile na kuchola uchanyha yake fana
munhu viyochola muhuli, ‘Yelile kwa Mndewa
Mulungu.’ 37 Chihande icho kwizachifunga
kwa luzabi kuulongozi wa chilemba cha bu-
luu. 38 Haluni kezachivala chihande icho kuna
ichihanga chake, kwa chihande icho kezasola
ubananzi uwatendile Waisilaili kuna ukunilavila
nhosa, niye Mndewa Mulungu nizazitogola nhosa
zawo. Haluni kezavala chihande icho lusita lose.
39 “Kwizamtengenezela Haluni joho
ditengenezigwe kwa walo dinogile na
kumuhogosela chilemba cha walo dinogile na
mkwiji utendigwe na fundi.

40 “Kwizawatengenezela wanage Haluni
majoho na mikwiji na kofiya muladi wawoneke
wana utunhizo na ukulu. 41 Kwizamvaza Haluni
ndugu yako na wanage mawalo yano, maabaho
uwahake mavuta na kwika kwa sang'hano yelile
na uwabagule muladi wanisang'hanile fana
wakulu wa nhambiko. 42 Iviya kwizawasonela
kaputula za chitani zondaziwagubike kwandusila
mchigudi mbaka muna yamawambo muladi
wagubike mwazi wawo. 43 Haluni na wanage
wezavala kaputula izo chila vondawengile muna

dihema da Mulungu hebu vondawawe habehi
na ulupango na kutenda sang'hano za ukulu wa
nhambiko hana ihanhu helile. Kwa kutenda ivo
hawezalagusa mwazi wawo na kukomigwa. Iyo
izakuwa ndagilizi ya siku zose kwa Haluni na
welesi wake.

# 29

### *Ndagilizi za kuwabagula Haluni na wanage fana wakulu wa nhambiko*

*(Walawi 8:1-36)*

1 “Vino niivo vondauwatendela Haluni na
wanage muladi kuwabagula wanisang'hanile
fana wakulu wa nhambiko. Sola dang'ang'a
da ng'ombe lume dimwe na mabebelu maidi
ya ng'hondolo yelibule chilema chochose,
2 na magate hayagumigwe lusu, maandazi
hayagumigwe lusu yabulugigwe na mavuta,
na magate masisili hayagumigwe lusu, mbali
yoigumigwe mavuta. Vinhu vino vose
vitengenenzigwe kwa usage lunhili wa ngano.
3 Maabaho uvike vinhu ivo muna ichigelo chimwe
na uvilave hamwe na diya dang'ang'a da ng'ombe
lume na ng'hondolo malume maidi.

4 “Maabaho wagale Haluni na wanage wa
chilume mbaka hana dihema da Mulungu na
uwanave na mazi. 5 Maabaho kwizasola yaja
mawalo ya ukulu wa nhambiko umvaze Haluni,
joho na ng'hanzu na chizibawo na chifuko cha
muimhambaga na kumzingiliza umkwiji uja
ubotigwe vinogile. 6 Mvaze Haluni chilemba
chiya muna iditwi na kwika chihande chiya
cha zahabu yelile uchanyha ya chilemba icho.

7 Maabaho sola mavuta yelile na umgidile mditwi
jake na umuhake.
8 "Maabaho wasole wanage na uwavaze
ng'hanzu, 9 na uwafunge mikwiji muna ivigudi
na kuwavaza kofiya zawo, vino ivo vondauweke
Haluni na wanage kwa sang'hano yelile. Wawo
wezakuwa wakulu wa nhambiko siku zose.
10 "Maabaho kwizagala dang'ang'a da ng'ombe
lume haulongozi ha hema da Mulungu. Haluni
na wanage wezakwika makono yawo uchanyha
ya ditwi da dang'ang'a da ng'ombe ijo. 11 Uchinje
dang'ang'a da ng'ombe ijo haulongozi ha Mndewa
Mulungu, hana ihanhu ha kwingilila muna di-
hema da Mulungu. 12 Kwizasola damu imwenga
ya ng'ombe na wiihake muna yamahembe ya ulu-
pango kwa chidole chako, damu yose yondaisi-
gale kwizaitila hasi ya ulupango. 13 Maabaho
kwizasola mavuta yose yogubika utumbo, hanhu
ha hasi ya maini hamwe na figo mbili na mavuta
yake, vose uvitimbule uchanyha ya lupango.
14 Mbali nyama ya dang'ang'a da ng'ombe lume ijo
na mbende na mavi yake kwizavisola na kuvitim-
bula kunze ya lago. Ino izakuwa nhambiko ya
uhasanyi.
15 "Maabaho kwizasola imwe mwa ng'ondolo
malume waja na umulongele Haluni na wan-
age weke makono yawo uchanyha ya ditwi jake.
16 Weye kwizamchinja na damu yake kwiza-
imizila banzi zose za ulupango. 17 Maabaho kwiz-
amkanha ng'hondolo lume iyo vihande vihande,
kwizasunha utumbo wake na migulu yake, uvike
vose hamwe na ditwi jake na vihande vake
vimwenga. 18 Maabaho kwizatimbula bebelu da

ng'hondolo ijo jose uchanyha ya lupango muladi kunilavila nhambiko ya kutimbuligwa, mnung'ho wa nhambiko yoitimbuligwa izaninogeza niye Mndewa Mulungu.
19 “Kwizasola ng'hondolo lume dimwenga, iviya Haluni na wanage wezakwika makono yawo uchanyha ya ditwi jake.
20 Kwizamchinja na kusola damu chidogo na kumuhaka Haluni na wanage hanhu ha hasi ha magutwi yawo ya kulume na muna yamadole ng'hulu da mikono yawo ya kulume na madole ng'hulu ya migulu yawo ya ukulume. Damu yondaisigale kwizalumizila ulupango banzi zake zose nne.
21 Maabaho kwizasola damu chidogo ili uchanyha ya ulupango hamwe na mavuta yaja yelile ummizile Haluni na mawalo yake, iviya uwamizile wanage na mawalo yawo. Haluni na wanage wezakuwa wela kumwangu hamwe na mawalo yawo yose.
22 “Kwizasola mavuta ya ng'hondolo lume, mkila wake na mavuta yogubika utumbo na hanhu hanonile hasi ha maini na figo zake mbili na mavuta yake, hamwe na chima cha kulume. Ng'hondolo iyo ni ng'hondolo wa kwikigwa kwa sang'hano yelile.
23 Muna ichigelo cha magate hayagumigwe lusu chili haulongozi wangu niye Mndewa Mulungu, kwizasola gate dimwe na andazi dimwe dodigumigwe mavuta na gate sisili dimwe.
24 Vinhu vino vose kwizamwing'ha Haluni na wanage muna yamakono yawo, nawo wezavinula uchanyha kuwa chilaguso cha kunilavila nhambiko niye Mndewa Mulungu.
25 Maabaho kwizavisola kaidi muna yamakono yawo na kuvitimbula uchanyha ya ulupango

hamwe na nhambiko ija ya kutimbuligwa, viwe mnung'ho unogile wouninogeza niye Mndewa Mulungu. Iyo ni nhambiko yoitimbuligwa kwa Mndewa Mulungu.

26 “Maabaho kwizasola chidali cha bebelu da ng'hondolo na kumwika Haluni kwa sang'hano yelile, na kuchinula uchanyha muladi kunilavila niye Mndewa Mulungu. Nacho chizakuwa chako.

27 “Kwika kwa sang'hano yelile ya ukulu wa nhambiko, vihande vidi va bebelu da ng'hondolo. Vino ivo chidali chinuligwe uchanyha na chima chibaguligwe. Chidali yeng'higwe Haluni, chima
weng'higwe wanage. 28 Ivo Waisilaili siku zose
wezasola vihande ivo kulawa muna zinhambiko zawo za tindiwalo zowonilavila niye Mndewa Mulungu na kumwing'ha Haluni na wanage, iyo ni nhambiko kwa Mndewa Mulungu.

29 “Haluni yahadanganika, mawalo yake yelile wezakwing'higwa welesi wake, nawo wezavala siku yawo ya kuhakigwa mavuta na kwikigwa
kwa sang'hano yelile. 30 Mwana wa Haluni yon-
dayawe mkulu wa nhambiko hanhu ha tati yake, kezavala mawalo yayo siku saba muna dihema da Mulungu, muladi yasang'hane usang'hano hanhu
helile. 31 Kwizasola nyama ya bebelu ijo da
kwikigwa kwa sang'hano yelile na kuikimusa
hana ihanhu hamwenga helile. 32 Haluni na
wanage wezakuja nyama ya bebelu ijo na gate dili muna ichigelo hanhu ha kwingilila muna di-
hema da Mulungu. 33 Wezakuja nyama izo zilav-
igwe kwa ichimu cha kuilumba na kwika kwa sang'hano yelile na kwa ichimu cha kuwabagula, mbali munhu imwenga sekeyalekeligwe kuja

nyama izo kwaviya zela. 34 One nyama yoyose
hebu magate yezasigala mbaka imitondo, basi
kwizaitimbula, sekeidigwe kwaviya yela.
35 "Ivo niivo vondauwatendele Haluni na
wanage kuisondelela na yaja yose yonikulagilize,
kwizaweka kwa sang'hano yelile kwa siku saba.
36 "Chila siku kwizalava ng'ombe lume dimwe
diwe nhambiko ya uhasanyi, kwa kutenda ivo
kwizalusafya ulupango, maabaho kwizachigidila
mavuta yelile muladi kulubagula ulupango.
37 Kwa siku saba kwizalusafya ulupango na
kulubagula. Uhakomeleza kutenda ivo, lupango
lwizakuwa lwela ng'hani na chinhu chochose
chondachidalise ulupango, chizakuwa chela.

*Nhosa za chila siku*

38 "Zino niizo nhambiko zomulondeka
kulava uchanyha ya lupango chila siku,
wanang'hondolo waidi malume weli na
mwaka umwe. 39 Mwanang'hondolo imwe
kwizamulava imitondo, mwanang'hondolo
imwenga kwizamulava ichigulogulo nguku
zikwingila. 40 Hamwe na mwanang'hondolo
wa mwanduso, kwizalava chibaba cha usage
lunhili wouhanganyigwe na lita imwe ya
mavuta yanogile na lita imwe ya divai fana
nhosa ya ching'waji. 41 Mwanang'hondolo
imwenga wa chigulogulo nguku zikwingila
kwizamulavila nhambiko hamwe na nhosa ya
usage na ya ching'waji fana viutendile imitondo,
mnung'ho wa nhambiko iyo yoilavigwa kwa moto
wizaninogeza niye Mndewa Mulungu.
42 "Nhambiko ino ya kutimbuligwa izalavigwa
siku zose, welesi mbaka welesi, haulongozi hangu

niye Mndewa Mulungu, haulongozi ha hanhu ha kwingilila muna dihema da Mulungu hondaniit-
ing'hane na kulonga na mweye. 43 Baho nizait-
ing'hana na wanhu wa Isilaili, baho hezakwela
kwa utunhizo wangu. 44 Nizabagula hema da Mu-
lungu na ulupango, iviya nizawabagula Haluni na wanage muladi wanisang'hanile fana wakulu wa
nhambiko. 45 Nizakala hagati ya wanhu wa Isi-
laili, na nizakuwa Mulungu wawo. 46 Baho weza-
vimanya kuwa niye niiyo Mndewa Mulungu, Mulungu wawo, yoniwalavile muna iisi ya Misili muladi nikale hagati yawo. Niye niiyo Mndewa Mulungu, Mulungu wawo.

# 30

### *Lupango lwa kusomela ubani (Kulawa 37:25-28)*

1 "Kwizatengeneza lupango lwa mibiki ya mkenge, kwa ichimu cha kusomela ubani.
2 Upango lwenyewo luwe lwa mulaba utali sentimita malongo mane na tano na ugalamu sentimita malongo mane na tano na chimo chake sentimita malongo kenda. Mahembe yake ya chila chingobweda yawe chinhu chimwe na
lupango lwenyewo. 3 Kwizachihaka zahabu
yelile, ubanzi wake wa uchanyha na banzi zake zose na mahembe yake, iviya kwizaitendela
lukingo lwa zahabu. 4 Kwizaitendela mhete mbili
za zahabu na kuziguma hasi muna ulukingo lwa mbavu zake mbili zoziilola, mhete izo zizasang'haniligwa kwamhilila mibiki lusita
lwa kuipapila. 5 Mibiki iyo iwe ya mkenge

na ihakigwe zahabu. 6 Lupango ulo lwike
haulongozi wa panzia haulongozi wa disanduku
da lagano, haulongozi ha ngubiko ya kuilumba,
hondaniiting'hane na weye.
7 “Chila imitondo Haluni viyosasala vitasa,
kezasoma ubani wili na mnung'ho unogile
uchanyha ya lupango. 8 Haluni kolondeka
kutenda ivo lusita voyokwacha vitasa
ichigulogulo nguku zikwingila. Nhosa ino
ya ubani izalavigwa siku zose kwa Mndewa
Mulungu bila kuleka muna zinyelesi zenu
zikwiza. 9 Muna ulupango luno, usome ubani
uluhusigwa muhala na sekemulave nhambiko ya
kutimbuligwa, hebu nhosa ya usage, hebu kugida
nhosa ya ching'waji uchanyha yake. 10 Haluni
kolondeka kuyasafya mahembe ya ulupango
mwanza umwe kwa mwaka. Kezayasafya kwa
damu ya nhambiko ya uhasanyi mwanza umwe
chila mwaka muna zinyelesi zenu zose, mana
lupango ulo lwela ng'hani kumwangu niye
Mndewa Mulungu.”

### *Kodi ya hema da Mndewa Mulungu*

11 Mndewa Mulungu kamulongela Musa,
12 “Vondauwapete Waisilaili, chila munhu
kezamuliha maliho Mndewa Mulungu kwa
ichimu cha ugima wake muladi hagati yawo
sekekuwe na mitamu ihile lusita lwa kupetigwa.
13 Chila munhu yopetigwa kolondeka yalihe nusu
shekeli ya hela, fana viipimigwe muna dihema
da Mulungu. Ino niiyo nhosa yondayanilavile
niye Mndewa Mulungu. 14 Chila munhu
yopetigwa kwandusila miyaka malongo maidi na

kugendelela, kezanilavila niye Mndewa Mulungu
nhosa iyo.
15 Tajili sekeyalave kufosa nudu
shekeli iyo ya hela hebu ngayengaye sekeyalave chidogo ya nusu shekeli iyo ya hela vomumulavila Mndewa Mulungu nhambiko ya kuilumba kwa ichimu cha ugima wenu.
16 Kwizahokela maliho
yayo ya kuilumba kulawa kwa Waisilaili na kwizayasang'hanila kwa sang'hano za hema da Mulungu, nayo yawe lukumbuso kwa Waisilaili haulongozi wangu niye Mndewa Mulungu muladi kuwatendelani kuilumba."

### *Ziga dodiumbigwe kwa shaba*

17 Mndewa Mulungu kamulongela Musa,
18 "Kwizatengeneza ziga dodiumbigwe kwa
shaba da kunawila dili na kalilo da shaba, udike hagati ya dihema da Mulungu na ulupango, na kudiguma mazi mgati yake.
19 Haluni na wanage
wezasang'hanila mazi yayo kunawa makono yawo na migulu yawo,
20 Lusita wang'hali
hawanakwingila muna dihema da Mulungu hebu kukwenhuka habehi ya lupango muladi kumulavila Mndewa Mulungu nhambiko za kutimbuligwa kwa moto. Wezatenda ivo muladi sekewadanganike.
21 Wolondeka
wanawe makono yawo na migulu yawo muladi sekewadanganike. Dino dizakuwa lagilizo jawo siku zose, kwandusila Haluni na wanage na kugendelela."

### *Mavuta yelile*

22 Mndewa Mulungu kamulongela Musa,
23 "Kwizasola vilungo vinogile ng'hani fana
vino, manemane ya mazi chilo sita, mdalasini

uli na mnung'ho unogile chilo nhatu, vilungo
vinung'hila goya chilo nhatu, 24 na modeli
imwenga ya mdalasini chilo sita, ningo izo zose
ziwe za kwiilinga na ningo za hema da Mulungu,
iviya uyahanganye na lita nne za mavuta ya
mzaituni. 25 Kwa vilungo ivo kwizatenda mavuta
yelile na uyahanganye fana munhu yokwenga
mavuta yonung'hila goya, mavuta yayo yela kwa
kuhaka. 26 Maabaho mavuta yayo kwizayagida
muna dihema da Mulungu na sanduku da lagano
27 na meza na via vake vose, chinala cha chitasa
na via vake, lupango lwa kusomela ubani 28 na
lupango lwa kutimbulila nhambiko na via vake
vose na ziga na kalilo jake. 29 Kwizavibagula
vinhu ivo, muladi veleng'hani. Chochose
chondachidalise vinhu ivo, chizakuwa chela.
30 Maabaho umuhake mavuta yelile Haluni na
wanage na kuwabagula muladi wanisang'hanile
fana wakulu wa nhambiko. 31 Walongele wanhu
wa Isilaili, 'Yano yezakuwa mavuta yangu yelile
ya kuhaka muna zinyelesi zenu zose. 32 Mavuta
yayo sekemumgidile munhu imwenga yoyose,
hebu sekemutengeneze mavuta yamwenga
yalingile yano, mavuta yano yela na lusita lose
yolondeka yele kumwenu. 33 Munhu yoyose
yondayenge mavuta fana yano hebu kumuhaka
munhu imwenga yoyose halondeka kuhakigwa
mavuta yano, kezawingigwa na wanhu wake.' ”

### *Ubani*

34 Mndewa Mulungu kamulongela Musa,
“Sola vilungo vino vili umulile, natafi na
shekelesi na kelibena, vilungo vili na mnung'ho

unogile, hamwe na ubani unogile. Vinhu
ivo vose viwe va ningo imwe. 35 Maabaho
kwizasang'hanila via ivo kutengenezela ubani
fana viutengenezigwa na munhu yotenda vinhu
vonhung'hila goya, ubani uli na munyu na mzelu
na wela. 36 Maabaho kwizaudunda uwe usage
lunhili muladi usang'haniligwe muna dihema da
Mulungu na kuwika haulongozi wa disanduku
da lagano, hanhu hondaniiting'hane na weye,
uwo kumwenu wizakuwa ubani welile ng'hani.
37 Sekemuitendele wenyewo ubani ulingile vino,
ubani uwo wizakuwa wela kumwenu haulongozi
wangu niye Mndewa Mulungu. 38 Munhu
yoyose yoitengenezela ubani ulingile uwo na
kuusang'hanila fana mavuta yonung'ha goya,
kezawingigwa na wanhu wake."

# 31

### *Wanhu wa kusasala hema da Mulungu (Kulawa 35:30-36:1)*

1 Mndewa Mulungu kamulongela Musa,
2 "Nimsagula Bezaleli, mwana wa Uli, mzukulu
wa Huli, kulawa kabila da Yuda, 3 na nimmemeza
Muhe wangu. Nimwing'ha udahi na kuzowela
na nzewele na umanyi wa kutengeneza vinhu,
4 muladi yatole sang'hano za umanyi, yahonde
zahabu na hela na shaba, 5 na kusongola mabwe
ya kuhamba na kusongola mibiki na kutenda
ufundi wa chila modeli. 6 Iviya nimsagula
Oholiabu mwana wa Ahisamaki, kulawa kabila
da Dani, yamtaze. Iviya niweng'ha udahi
mkulu wanhu wamwenga kwa ichimu cha
sang'hano mbasakanyo, muladi watengeneze

vinhu vose vinikulagilize. 7 Watengeneze hema
da Mulungu na sanduku da lagano na ngubiko
iyo ya kuilumba ili uchanyha yake, hamwe na
via vake vose, 8 meza na via vake na chinala
cha chitasa na via vake vose na lupango lwa
kusomela ubani, 9 lupango lwa kutimbulila
nhambiko na via vake vose, ziga na kalilo jake,
10 na mawalo yabotigwe vinogile, mawalo yelile
ya mkulu wa nhambiko Haluni na mawalo ya
wanage wondawatende sang'hano ya ukulu
wa nhambiko, 11 mavuta yelile na ubani wili
na mnung'ho unogile kwa ichimu cha hanhu
helile. Vinhu ivo vizatengenezigwa fana viya
vinikulagilize."

### *Siku ya Mhumulo*

12 Mndewa Mulungu kamulongela Musa,
13 "Walongele wanhu wa Isilaili, 'Izindilileni siku
yangu ya Mhumulo, mana chino ni chilaguso
hagati ya niye na mweye kwa nyelesi zenu
zose, ivo mwizavimanya kuwa kweli niye
niiyo Mndewa Mulungu, yonimtendani mwele.
14 Molondeka muizindilile Siku ya Mhumulo,
kwaviya yela kumwenu. Munhu yoyose yoitenda
siku iyo yambule mwiko, kolondeka yakomigwe.
Munhu yoyose yosang'hana usang'hano siku
iyo, kolondeka yawingigwe na wanhu wake.
15 Sang'haneni sang'hano zenu kwa siku sita,
mbali siku yesaba ni siku ya kuhumula ni yela,
siku iniibagule niye Mndewa Mulungu. Munhu
yoyose yosang'hana usang'hano muna Isiku ya
Mhumulo, kolondeka yakomigwe. 16 Waisilaili
waizindilile Siku ya Mhumulo na waitende

kwa nyelesi zawo zose fana viya lagano da siku
zose. 17 Chizakuwa chilaguso hagati ya niye na
Waisilaili siku zose, mana niye Mndewa Mulungu
nilumba ulanga na isi kwa siku sita, mbali
siku yesaba nileka kusang'hana usang'hano na
nihumula.' ”
18 Mndewa Mulungu viyakomeleze kulonga
na Musa kuna mulima wa Sinai, kamwing'ha
Musa vibawo vidi va mabwe ya ukalangama,
vandikigwe malagilizo kwa chidole cha Mulungu
mwenyewo.

# 32

### *Nyang'hiti ya dang'ang'a da zahabu (Kumbukumbu 9:6-29)*

1 Wanhu viwawonile Musa kakalama
kuhumuluka kulawa kuna mulima, waiting'hana
kumzunguluka Haluni na wamulongela,
“Chitengenezele nyang'hiti za milungu
yondaichilongoze. Musa yoyachilavile kuna iisi
ya Misili, hachivimanyile kapatigwa na choni.”
2 Haluni kawedika, soleni heleni za zahabu muna
yamagutwi ya wake zenu na wanenu, munigalile.
3 Ivo wanhu wose wahambula heleni zawo za
zahabu na wamgalila Haluni. 4 Haluni kazihokela
kulawa muna yamakono yawo na katengeneza
dang'ang'a lume da wa ng'ombe wa zahabu.
Wanhu walonga, “Weye Isilaili, ino iyo mulungu
wetu, yoyachilavile kuna iisi ya Misili!”
5 Maabaho Haluni viyawonile ivo, kazenga lu-
pango haulongozi ha didang'ang'a na kalonga,
“Igolo kwizakuwa na dugila da kumuhishimu Mn-
dewa Mulungu.” 6 Igolo yake wanhu waidawa

walava nhambiko za kutimbula na nhambiko za
tindiwalo. Wanhu wakala hasi kuja na kung'wa,
maabaho wema na kuvina.

7 Maabaho Mndewa Mulungu kamulongela
Musa, “Humuluka, kwaviya wanhu wako
wouwalavile kuna iisi ya Misili wahasanya.
8 Waileka nzila ija yoniwalagilize kuisondelela,
watenda dang'ang'a lume da zahabu na
kuditambikila na kudilavila nhosa, wolonga,
‘Weye Isilaili, ino niiyo mulungu wetu,
yoyachilavile kuna iisi ya Misili!’ ” 9 Mndewa
Mulungu kamulongela Musa, “Niwawona
wanhu wano, wana mizoyo midala. 10 Lelo
sekeunigomese, nileke niwadanganize kwa
ludoko lwangu. Maabaho kufosela weye,
nizatenda wanhu wa kabila kulu.”

11 Mbali Musa kamulamba Mndewa Mulungu,
Mulungu wake, kamulongela, “Weye Mndewa
Mulungu, habali kuna ludoko na wanhu wako
wouwalavile kuna iisi ya Misili kwa udahi wako
mkulu na mkono wako uli na ludabwa? 12 One
uhatenda ivo, Wamisili wezadaha kulonga kuwa
kawalava muna iisi ya Misili muladi kuwakoma
muna mulima na kuwananga. Galula magesa
yako ya ludoko na sekeuwatende wanhu wako
mbuli zihile. 13 Wakumbuke wasang'hani wako,
Bulahimu na Isaka na Yakobo, wouwalahile kwa
kulonga, ‘Nizakongeza welesi wenu fana nhondo
za kuulanga na nizaweng'ha welesi wenu isi ino
yose yonimulahileni kuweng'ha, izakuwa yawo
siku zose.’ ” 14 Mndewa Mulungu kagalula
magesa yake ya kuwatendela wanhu wake mbuli
zihile zoyalongile.

15 Maabaho Musa kahumuluka kulawa kuna
mulima kuno kamha vibawo vidi va mabwe va
ukalangama muna yamakono yake, vandikigwe
banzi zose. 16 Vibawo ivo vikala sang'hano ya
Mulungu, mwandiko wandikigwa na Mulungu
mwenyewo.
17 Yoshua viyahulike madizi ya wanhu woguta,
kamulongela Musa, “Nohulika dizi da ng'hondo
muna dilago.”
18 Musa kamwidika, “Siyo dizi da kuhuma hebu
kuhumwa, mbali dizi da wanhu wokwimba.”
19 Musa viyafikile mudilago na kuwona
dang'ang'a na wanhu wovina, kawona ludoko
ng'hani. Kavasa ivibawo viya kulawa muna
yamakono yake na kuvibena haja hasi ya mulima.
20 Kasola dang'ang'a lume dowatendile na
kadisoma moto, maabaho kadidunda mbaka
diwa usage, kakologa usage uwo muna yamazi
na kawawangiliza Waisilaili wang'we. 21 Musa
kamuuza Haluni, “Wanhu wano wakutenda
choni mbaka kuwatenda watende uhasanyi
mkulu ivo?”
22 Haluni kamwidika, “Sekeuniwonele ludoko
niye msang'hani wako. Kuwamanya wanhu
wano viwaisasale kutenda yehile. 23 Wanilongela,
‘Chitendele milungu yondaichilongoze. Musa
